# Nipashe

Jumatatu Agosti 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581416

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




NIPASHE JUMATATU AGOSTI 28, 2023

Nipashe Spotika

TASHA12 AKUNWA NA VIPAJI, UKURASA 14

€87.5 MILLION PER SEASON

ISIKUPITE

Ilikuwa siku iliyojaa ushindi na dhiki kwa mshambuliaji nyota wa Arsenal Bukayo Saka baada ya winga huyo mwenye umri wa miaka 21 kuvunja rekodi ya Paul Merson ambayo ilidumu kwa miaka 26, ya kucheza mechi 82 mfululizo kwa kucheza mechi yake ya 83 mfululizo. Lakini katika hali ya ukatili wa kejeli, Saka alifanya kosa kwa kumpasia Andreas Pereira, aliyeitanguliza Fulham kupata bao wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Emirates juzi.

TIMU SABA ZINAZOONGOZA MIKATABA MINONO YA JEZI

LONDON, England

KLABU za soka zilizingia mikataba ya udhamini na chapa za nguo za michezo ili kuzalisha na kusambaza vifaa vya timu na bidhaa nyinginezo. Hiki ni chanzo kikubwa cha mapato kwa klabu za soka kwani mikataba hii inazisaidia kuzalisha kiasi kikubwa kupitia chapa na uuzaji.

Dili la jezi kwa kawaida huhusisha jezi za klabu, vifaa vya mazoezi, mavazi mengine na bidhaa mbalimbali za mashabiki. Jumla ambayo chapa inalipa kwa mpango kama huo inaweza kutofautiana kulingana na umaarufu wa klabu ulimwenguni na mafanikio yake.

Ofa za vifaa si tu huchangia uimara wa kifedha wa klabu, lakini huchangia katika kuunda utambulisho wake na utambuzi wa chapa. Hii ni kwa sababu muundo au mwonekano wa seti ya timu inakuwa sehemu muhimu ya uwakilishi wake wa kuona.

Acha sasa tuangalie timu saba zilizo na ofa kubwa zaidi za jezi zinazolipwa kwa msimu...

#7 Chelsea - Euro milioni 70 kwa msimu (Nike)

Chelsea ilitia saini mkataba wa jezi na miamba ya nguo za michezo ya Nike ambao ulianza kutekelezwa msimu wa 2017-18. Ndio mkataba mkubwa zaidi wa kibiashara katika historia ya klabu hiyo ya Ligi Kuu England. Mkataba huo una thamani ya Euro milioni 70 kwa msimu na utaendelea kwa miaka 15 kutoka mwaka 2017.

Kabla ya kusaini mkataba huo, Chelsea ilipunguza mkataba wa Adidas uliokuwepo kwa miaka sita. Mkataba huo na kampuni ya Nike uliripotiwa kuongeza maradufu mapato ya 'The Blues' hao kutokana na makubaliano yao ya awali na Adidas.

#6 Manchester City - Euro milioni 75 kwa msimu (Puma)

Hili ndiyo dili pekee kati ya 10 zilizoingiza fedha nyingi zaidi duniani ambazo hazihusishi Adidas au Nike. Manchester City walitia saini mkataba huo mwaka 2019 na thamani yake ni Euro milioni 75 kwa msimu. Hata hivyo, kwa kuwa mkataba huo una miaka minne sasa na City ilishinda mataji matatu msimu uliopita, huenda ukaongezwa tena.

Mashabiki wa City wameonekana kufurahishwa na jezi ambazo Puma wameweka katika misimu ya hivi karibuni. Lakini wakati huo huo, kimekuwa kipindi kizuri cha mafanikio kwa City na mashabiki huwa hawalalamiki chochote wakati kabati ya vikombe inapokuwa imejaa.

#5 Paris Saint-Germain - Euro milioni 80 kwa msimu (Nike)

Umaarufu na mafanikio ya Paris Saint-Germain kwenye jukwaa la kimataifa, pamoja na kikosi chao chenye nyota wengi, uliwafanya kuwa mshirika muhimu wa Nike. PSG wameweza kusajili baadhi ya wanasoka bora duniani kama Lionel Messi, Neymar na Kylian Mbappe katika miaka ya hivi karibuni.

Umaarufu wao katika kiwango cha kimataifa umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika muongo uliopita na imekwenda mbali sana kuwasaidia kupata mkataba wa faida wa vifaa vya Nike.

#4 Arsenal - Euro milioni 85 kwa msimu (Adidas)

Adidas waliongeza mkataba wao wa jezi na Arsenal Septemba mwaka jana. Kwa mujibu wa makubaliano mapya, wataendelea kutengeneza na kusambaza vifaa vya 'Washikabunduki' hao hadi 2030. Kwa mujibu wa masharti ya mkataba huo mpya, Arsenal itaingiza euro milioni 85 kwa msimu kutoka Adidas.

Adidas na Arsenal zimeripotiwa kuangazia kuwekeza katika kutengeneza safu za bidhaa kwa wachezaji na mashabiki wa kandanda na pia kuwekeza katika jamii za wenyeji.

#3 Manchester United - Euro milioni 87.5 kwa msimu (Adidas)

Manchester United wameweka kalamu kwenye mkataba wa jezi kubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu England. Mkataba huo mpya utaendelea hadi mwaka 2035 na unawakilisha nyongeza ya miaka 10 kwenye makubaliano yao ya sasa na Adidas.

Kwa mujibu wa mkataba huo mpya, Manchester United itaingiza kiasi cha Euro milioni 87.5 kwa mwaka, na kuwafanya kuwa wanaolipwa fedha nyingi zaidi kupitia udhamini wa jezi kwenye Ligi Kuu England.

#2 Barcelona - Euro milioni 105 kwa msimu (Nike)

Nike imekuwa msambazaji rasmi wa jezi za Barcelona tangu mwaka 1998. Pande zote mbili zimeonesha nia ya kufanya kazi pamoja na hii imesaidia uhusiano wao kukua kwa miaka mingi. Mnamo 2018, Barca iliongeza mkataba wao na Nike kwa miaka 10.

Kwa mujibu wa mkataba huo mpya, Barcelona wanapata euro milioni 105 kwa msimu kutoka kwa Nike. Ni dili la pili kwa bei ghali zaidi katika historia ya mchezo huo mzuri.

#1 Real Madrid - Euro milioni 120 kwa msimu (Adidas)

Kama vile Barcelona na Nike, Real Madrid na Adidas wamekuwa na ushirikiano tangu mwaka 1998. Ushirikiano huo unatazamiwa kuendelea hadi mwaka 2028 kulingana na masharti ya makubaliano yaliyokubaliwa kati ya pande hizo mbili mnamo mwaka 2019.

Real Madrid itapokea kitita cha Euro milioni 120 kwa msimu kutoka kwa Adidas na ni dili la jezi zenye faida kubwa zaidi katika historia ya soka.

UKURASA 11


tigo pesa SportPesa

MAOKOTO Deilee!

WEKA ZAIDI,BET USHINDE ZAIDI

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mwinyi** azindua ujenzi wa kituo cha afya chenye hadhi maalum

UKURASA 17

# Miradi yenye ajenda za kuharibu maadili

• **Rais** Samia awapa angalizo ma-RC, ma-RAS kuwalinda vijana... *Ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali wakati akifunga mafunzo ya wakuu wa mikoa pamoja makatibu tawala wa mikoa katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha kwa Mfipa, Pwani jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### MBARONI TUHUMA KUJIHAMISHIA MIL. 4/- ZA MTEJA AKIMSAJILIA 5G

JESHI la Polisi mkoani Songwe linamshikilia, Kelvin Greeton (23), mkazi wa Isanga, mkoani Mbeya, kwa tuhuma za wizi wa Sh. milioni nne za mteja aliyekuwa akimsaidia kusajili laini mpya ya simu ya mkononi kutoka mtandao wa 4G kwenda 5G...

UKURASA WA 7

### LHRC YATOA ANGALIZO KANUNI SHERIA YA HABARI



MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, ameshauri Kanuni za Sheria ya Huduma...

# Wahitimu 760 BBT kupewa mashamba, kunolewa JKT siku 30

UKURASA 3

# TMA yatoa tahadhari upepo mkali siku tano

UK.2

**MICHEZO** GAMONDI AIANZIA KAZI AL-MERRIKH UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Himiza Development Organization (HDO), lenye masikani yake Mkuranga mkoani Pwani, Prisca Ngwesgemi (kushoto), akiendesha mafunzo ya malezi bora kwa wakazi wa Kata ya Mbagala Kuu Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Samia awapa angalizo ma-RC, ma-RAS miradi inayoharibu maadili kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewaagiza wakuu wa mikoa (ma-RC) na makatibu tawala wa mikoa (ma-RAS) kuendana na mabadiliko ya dunia.

Vilevile, amewataka kuhakikisha usalama wa vijana kwa kusimamia miradi inayowahusisha ambayo mingi hutumika kupenyeza ajenda zinazopotosha maadili na utamaduni wa taifa.

Rais Samia alitoa maagizo hayo jana wakati akifunga mafunzo kwa viongozi hao katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, wilayani Kibaha, mkoani Pwani, yakiandaliwa na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Alisema ni muhimu kila kiongozi akawa mwepesi kukabiliana na mabadiliko hayo ili kuendana na mfumo wa dunia wa sasa na kiuchumi bila kusubiri maelekezo kutoka juu.

"Kuna tabia ya 'kujidogosha', kujifanya 'mimi ninasubiri maelekezo ya juu, sifanyi maana ninasubiri juu', juu kwa nani? Pale ulipo juu ni wewe, kuna watu wanasubiri maelekeo ya juu pale ulipo.

"Muwe 'active' kuangalia mikakati, mbinu, serikali inasema nini na ninyi mnakwenda haraka na mabadiliko, tukifanya hivyo tutakwenda na maendeleo haraka.

"Kwenye uongozi, kuna muundo tofauti tofauti, mimi sitakushushia nini cha kusema, ninataka wewe uwe na ndoto zako, nini unataka kufanya kulingana na sheria, kanuni, miongozo, mipango na mikakati ya serikali, yote kwenye eneo lako unaitumiaje kutimiza katika eneo lako, usisubiri Rais asema Mkuu wa Mkoa fanya hilo, kila kiongozi na muundo wake.

"Mimi ninapenda kuona mtu anajituma, anajielewa na anajua nini anafanya. Huyumbishwi katika nafasi yako. Ninataka kuona kila mtu kasimama kwenye nafasi yake, ikitokea mtu amekupa changamoto kwenye uamuzi wako, uwe na hoja ya kutetea, amekuja mkubwa unajitetea na unasimama kwenye uamuzi wako.

"Ninaposema kusimama siyo muwe kichwa ngumu kwamba Rais kasema nisimame kwenye uamuzi wangu. Ninachotaka ni hiki. Hatuendi hivyo," alisema.

Rais Samia pia aliwaagiza viongozi hao kuacha kupuuza wananchi, hivyo wawatumikie kwa kuwapa huduma na kushughulikia kero, malalamiko na mahitaji yao.

Mkuu wa Nchi pia aliwataka watumishi serikalini katika idara tofauti kwenye ngazi za mikoa, kutumia fedha za maendeleo zinazotolewa kwa maslahi ya wananchi.

Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, alimshukuru Rais kwa mpango kazi wa viongozi kupata mafunzo ya uongozi ambayo yataboresha mpango kazi.

Alisema mfumo huo una tija kubwa kwa kuwa umeshaleta matokeo ya mabadiliko ya kiutendaji katika maeneo mbalimbali.

Alimhakikishia Rais Samia kuwa wataendelea kusimamia miradi yote iwe ya viwango na kukamilika kwa wakati ili iwe mtatuzi wa kero za wananchi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, aliwataka wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kusimamia ipasavyo biashara katika maeneo yao na kuwazuia watendaji wa taasisi za serikali kufunga biashara za watu na kusababisha mizozo katika ukusanyaji kodi, tozo na mambo mengine kwa kuwa hatua za kufunga biashara na ofisi hizo zina athari kubwa kiuchumi na ajira za watu.

"Utaratibu huu unakwenda kinyume cha juhudi kubwa za Rais Dk. Samia kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini. Nilielekeza na ninaendelea kusisitiza kuwa ni marufuku kwa taasisi yoyote ya serikali kufunga biashara, ofisi ama maeneo yoyote ya uzalishaji kwa kigezo cha kukiuka taratibu mbalimbali.

"Mwenye biashara achukuliwe hatua kwa makosa ya biashara na siyo kuifunga biashara yenyewe," alisisitiza Dk. Nchemba.

Pia aliwahimiza viongozi hao wa mikoa kuweka usimamizi madhubuti wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika maeneo wanayoyasimamia, ili kufikia malengo na kuwezesha mipango ya serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya utoaji huduma za msingi za kijamii ikiwamo elimu, afya na maji safi na salama.

Alisema kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, serikali inatarajia kukusanya Sh. trilioni 44.39 kutoka vyanzo vyote. Kati yake, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya halmashauri yanatarajiwa kuchangia asilimia 70.7, misaada na mikopo nafuu asilimia 12.3 na mikopo ya kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi asilimia 17.

Aliagiza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) na kuhakikisha miradi inayoibuliwa na kutekelezwa, inakuwa na tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kukagua thamani ya fedha iliyotumika na viwango vinavyotakiwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Angellah Kairuki, alisema mafunzo hayo yanatakiwa kwenda kuleta mabadiliko katika ukusanyaji mapato na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha.

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alisema mafunzo hayo yanakwenda kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa viongozi hao.

Alisema fursa waliyoipata viongozi hao itaongeza kasi ya utatuzi wa kero za wananchi, sambamba na kutekeleza ahadi ya chama hicho ya kuboresha huduma kwa wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia, Sh. trilioni 1.15 zimepokewa katika mkoa huo na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

# TMA yatoa tahadhari upepo mkali siku tano

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA) imewatahadharisha wakazi wa Pwani ya Bahari ya Hindi na maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa kuhusu kuwapo na upepo mkali na mawimbi makubwa kwa siku tano kuanzia leo.

Kupitia ukurasa wa kijamii wa Instagram, TMA ilieleza kuwa upepo huo unatarajiwa kufikia kilomita 40 kwa saa na mawimbi makubwa kufikia mita mbili yakiwa na uwezekano wa kuleta athari katika maeneo hayo.

Aidha, ilieleza kuwa madhara yanayoweza kutokea katika maeneo hayo ni kuathirika kwa baadhi ya shughuli za uvuvi na usafirishaji wa baharini na kuwataka wanaofanya shughuli hizo kuwa na tahadhari.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa leo na kesho maeneo yanayoweza kupata athari za wastani kwa ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ni mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba.

Kwa ukanda wa Ziwa Victoria taarifa hiyo ilitaja mikoa inayoweza kuathirika ni Kagera, Geita, Mwanza, Mara na Simiyu, ukanda wa Ziwa Tanganyika ni mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa na ukanda wa Ziwa Nyasa ni Mbeya, Njombe na Ruvuma.

Aidha, TMA ilieleza kwa siku ya Jumatano maeneo yanayoweza kuathiriwa na hali hiyo ni ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ambayo ni mikoa ya Lindi, Mtwara, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, viziwa vya Mafia, Unguja na Pemba.

Mtafiti mbobezi wa viumbe bahari kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Prof. Philip Bwathondi, aliwashauri wavuvi na wasafirishaji kusitisha shughuli kwa siku zilizotangazwa na TMA ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea ikiwamo boti kuzama, kujeruhi na kusababisha vifo kwa wavuvi.

Vilevile, alisema kunapokuwa na upepo mkali baharini na mawimbi makubwa nguvu ya mkondo inaongezeka na kuleta athari kwa wavuvi kupelekelkwa eneo tofauti na wanapotega nyavu zao, hata kusababisha baadhi yao kupelekwa kwenye kina kirefu.

Aidha, alisema mawimbi yanapokuwa makubwa samaki wanajificha kwenye matumbawe na upatikanaji wao unakuwa wa shida kwa kuwa nao pia wanakimbia machafuko.

Alisema wakati mwingine upepo mkali husababisha mvua, kama wavuvi wanakwenda kuvua wanapata usumbufu wa kunyeshewa.

Katibu wa Wavuvi wa Mwalo wa Buyuni (BMU), Musa Kayanda, alisema wameisikia taarifa hiyo kupitia vyombo vya habari na kama hali itakuwa kama ilivyotangazwa hawatokwenda kufanya shughuli za uvuvi kujiepusha na majanga.

Alisema kwa hali hiyo huwa inatokea kwa miezi ya Julai na Agosti na kudumu kwa siku tatu hadi tano na kuathiri shughuli zao za kujiingizia kipato kupitia uvuvi.

Mvuvi kutoka mwalo wa samaki wa Kunduchi, Sadiki Chale, aliishauri TMA kutafuta namna bora ya kufikisha taarifa kama hizo kwa wavuvi ambao ni waathirika wakubwa wa machafuko ya bahari kuliko kutangaza kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari pekee kwa kuwa siyo wote wanaoweza kupata taarifa hizo.

Wakati huo huo, Mamlaka hiyo imewataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na mvua ya El-Nino zinazotarajiwa kunyesha mwezi Oktoba hadi Desemba.

Imesema kutokana na mvua hiyo kunatarajiwa kuwapo mafuriko na maporomoko ya ardhi na kuleta madhara makubwa kwa binadamu na mazingira, ikiwamo matukio ya vifo, magonjwa ya mlipuko na uharibifu wa miundombinu na upotevu wa mali.

Mamlaka hiyo imezishauri sekta na taasisi mbalimbali, zikiwamo za kilimo, mifugo, uvuvi, utalii, wanyamapori, uchukuzi, mamlaka za miji, nishati, maji na madini, sekta binafsi, Wizara ya Afya na menejimenti za maafa kuchukua hatua mapema kabla ya kuanza kwa mvua hizo.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kujihamishia mil. 4/- za mteja akimsajilia 5G

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

JESHI la Polisi mkoani Songwe linamshikilia, Kelvin Greeton (23), mkazi wa Isanga, mkoani Mbeya, kwa tuhuma za wizi wa Sh. milioni nne za mteja aliyekuwa akimsaidia kusajili laini mpya ya simu ya mkononi kutoka mtandao wa 4G kwenda 5G.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa Agosti 21 mwaka huu baada ya kutenda kosa hilo kupitia simu ya mteja wake kinyume cha sheria.

"Mtuhumiwa huyu ambaye pia ni dereva wa bajaji, ni miongoni mwa vijana waliokuwa wanatafutwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za makosa ya kimtandao.

"Wamekuwa wakitumia kivuli cha kusajilia wateja laini mpya za simu kutoka 4G kwenda 5G na baadaye kufanya wizi kwa kuhamisha fedha zilizomo katika simu hizo za wateja au zilizounganishwa na mifumo ya benki," alifafanua Kamanda Mallya.

Alisema mtuhumiwa huyo baada ya kubanwa, alikiri kosa hilo kupitia kujua namba za siri za mteja wake ndipo alipojihamishia kiasi hicho cha fedha kilichokuwa kimehifadhiwa katika akaunti ya Benki ya NMB.

Kamanda Mallya alisema jeshi hilo linaendelea na uchunguzi na pale utakapokamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Jeshi hilo pia linamshikilia Willium Mpenda (34), mkazi wa Jiji la Mbeya, kwa tuhuma za kuvunja na kuiba Sh. milioni 10, simu 120, vocha za mitandao mbalimbali na mali nyingine katika maduka matatu tofauti Mtaa wa Vibanda wa Kituo cha Malori, mjini Vwawa, wilayani Mbozi.

"Mtuhumiwa ambaye bado tunaendelea kutafuta mtandao anaoshirikiana nao katika tukio hilo, baada ya kufanikiwa kutoboa bati juu ya paa katika duka moja na kutumbukia ndani, alikusanya mali zilizokuwapo ndani ya duka hilo na kuingia katika maduka mengine mawili kwa kuwa yalikuwa yameungana," alifafanua Kamanda Mallya.

Kamanda Mallya alisema kuwa baada ya mtuhumiwa kukamatwa na kufanyiwa upekuzi, alikutwa na baadhi ya mali hizo za wizi ambao ni simu sita na vocha mbalimbali za mitandao ya simu zenye thamani ya Sh. 65,000.

Alisema katika mahojiano, mtuhumiwa huyo alikiri kosa hilo. Fedha alizopata, alinunua pikipiki yenye namba za usajili MC 537 DXZ. Inashikiliwa na jeshi hilo.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati), Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa pili kushoto) na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete (wa pili kulia), wakimsikiliza Mkurugenzi wa Shirika la Madini (STAMICO), Venance Mwasse (kushoto), walipotembelea banda la shirika hilo na kuzungumzia madini ya chumvi kwenye maonyesho ya madini na fursa za uwekezaji yaliyofanyika Mjini Ruangwa mkoani Lindi juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wahitimu 760 BBT kupewa mashamba, kunolewa JKT

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ametangaza neema kwa wahitimu 763 wa Programu ya Jenga Kesho Bora (BBT) kugawiwa mashamba kesho katika eneo la Chinangali na Ndgogye, mkoani Dodoma.

Vijana hao pia wanatakiwa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kupewa mafunzo ya kizalendo kwa mwezi mmoja.

Akizungumza na wahitimu hao jana jijini hapa, Bashe alisema katika mgawanyo wa mashamba hayo, wanawake watakabidhiwa mashamba eneo la Chinangali na wanaume eneo la Ndogoye.

Waziri Bashe alisema kuwa baada ya kutoka JKT, watarejea katika maeneo ya mashamba yao kwa ajili ya kuanza kilimo Oktoba mwaka huu.

"Watakaporejea katika mashamba yao, watakuta tayari kwa ujenzi wa nyumba ambazo wataishi wakiwa wanafanya kilimo biashara. Hawa ndio wapigania uhuru wa BBT.

"Serikali itakuwa pamoja nao kuwashika mkono kwa mwaka mmoja. Baada ya hapo wataendelea kusimama wao wenyewe kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha biashara na chenye tija," alisema Bashe alisema kuwa baada ya mwaka, serikali itawaacha wafanye kilimo wenyewe lakini hawatoruhusiwa kuuza mashamba.

Waziri huyo alisema serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya umwagiliaji ili kuhakikisha wahitimu hao wanaokwenda kuanza kilimo, wanafanya kilimo chenye tija ili kuwa mfano wa kuigwa.

Kuhusu bima ya afya, Waziri Bashe alisema majina yao yamewasilishwa kushughulikiwa kupata bima ili kila mhitimu awe na uhakika wa matibabu.

"Suala la bima ya afya pamoja na fedha za kujikimu ninakwenda kulifanyia kazi ila ninawahakikishieni yote yanakwenda kutimia ikiwamo kupewa smart card ambayo itakuwa ina taarifa zote za wakulima na serikali itaendelea kuwa pamoja na ninyi," alisema Bashe.

Waziri huyo alibainisha kuwa awali baadhi ya watu waliona kama programu hiyo watu wanakwenda kucheza lakini baadhi ya nchi za Afrika wamekuja kutembelea na kujifunza ili kuitekeleza katika nchini zao.

Kuhusu mikopo, Bashe alisema benki nyingi zimeanza kujitokeza kutoa mikopo kwa ajili ya kuwakopesha vijana hao ikiwamo NMB. Mratibu wa programu hiyo, Vumilia Zikankuba, alisema vijana hao wako tayari kuanza kilimo kwa lengo la kuiheshimisha programu hiyo.

Machi 20 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan akizindua programu hiyo, alisema ni mwanzo wa safari ya kufikia mwaka 2030, kilimo kitapokuwa kinachangia asilimia 10 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 3.6.

Julai 10 mwaka huu, akiwa katika maadhimisho ya miaka 60 ya JKT, Rais Samia alisema serikali itaunganisha BBT na kambi za mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kuongeza fursa za vijana kujitegemea na kushiriki shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.

"Lengo la serikali ni kuunganisha shughuli zinazofanywa na JKT kuingia katika mpango huu. Tunaposema tunakwenda kukarabati kambi zaidi, kambi tunazokwenda kuzirekebisha zitaunganishwa katika mpango wa BBT, ili kujenga kesho nzuri ya vijana.

"Serikali imedhamiria kuiwezesha JKT kuwa ya kisasa zaidi yenye kuendana na mahitaji ya sasa katika kutimiza majukumu ya malezi ya vijana, kuwajenga uzalendo wenye kulithamini taifa, kujitegemea uzalishaji mali na kulitetea Taifa bila hofu," alisema.

# Operesheni yanasa kilo 270 za dawa za kulevya Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, imefanya operesheni maalum katika Mkoa wa Iringa na kukamata kilo 276 za dawa za kulevya aina ya heroin na bangi, huku watu 12 wakikamatwa kwa tuhuma za kuhusika na dawa hizo.

Akitoa taarifa kwa niaba ya Kamishna Jenerali, Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa Mamlaka hiyo, Daniel Kasokola, alisema jana kuwa lengo la operesheni hiyo ni kuvunja na kusambaratisha mitandao yote ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya na kuwakamata wote wanaojihusisha ili wachukuliwe hatua za kisheria.

"Operesheni hizi ni moja ya utekelezaji wa mkakati wa kudhibiti upatikanaji wa dawa za kulevya, hivyo kama Kamishna Jenerali anavyoeleza, operesheni hizi zitafanyika nchi nzima.

"Tuwahakikishie tutawakamata vinara wote wanaojihusisha kwa namna moja au nyingine na kilimo au biashara ya dawa za kulevya kwa kuwa mitandao yao na mbinu zao tunazijua. Hakuna mhalifu wa dawa za kulevya ambaye ataukwepa mkono wa sheria," alionya.

Kasokola alisema serikali imejipanga kikamilifu kukabiliana na dawa za kulevya nchini, hivyo, kwa sasa Tanzania siyo sehemu salama kwa wote wanaojihusisha na biashara au kilimo cha dawa za kulevya.

Hivyo, aliwataka Watanzania waungane na serikali katika mapambano hayo kama walivyofanya wananchi wa Kisimiri Juu, Lesinoni na Lenglong mkoani Arusha na wananchi wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro kuamua kwa hiari yao kuondoa mimea ya bangi na mirungi katika maeneo yao.

Pia alisema dawa za kulevya zina madhara makubwa kwa taifa, ikiwamo kiafya, kijamii, kiuchumi, kiusalama na kidiplomasia. Alisema katika kukahakikisha dawa za kulevya zinazibitiwa, Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015 inatoa adhabu kwa wale watakaotiwa hatiani kwa makosa hayo. Ni adhabu ya hadi kifungo cha miaka 30 gerezani au kifungo cha maisha pamoja na kutaifishwa mali zote za mshtakiwa ambazo zitathibitika alizipata katika kipindi cha miaka 10 tangu akamatwe.

Mtendaji wa Kata ya Malolo, Wilaya ya Kilosa, Fredinand Litweka, alipongeza kufanywa operesheni hiyo katika maeneo hayo, akiyataja yameshamiri kwa kilimo cha bangi.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**
**BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA**
**SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA**
**Ofisi ya Mkurugenzi,**
**OFISI ZOTE: +255 736 200911/12**
**Manispaa ya Ilemela,**
**FAX: +255 028 736 200910**
**E-mail: IlemelaMunicipal@yahoo.com MWANZA**

**Kumb.Na.IMC/L/16953/12/SBM**
**Tarehe: 24/08/2023**
**Kwa yeyote anayehusika,**
**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO (LETTER OF OFFER) YA KUMILIKI ARDHI .**

**Offer ya kiwanja Na. 278 Kitalu 'G' NYAMANORO.**
Mmiliki aliyeandikishwa: **HUSSEIN HASSAN LUGWISA** wa S.L.P 875, Mwanza.

Muombaji: **SHANI HUSSEIN LUGWISA** wa S.L.P 875, Mwanza.

**TAARIFA IMETOLEWA** kwamba offer ya mmiliki wa ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea, na ninakusudia kutoa offer mpya badala yake iwapo hakuna pingamizi lolote kwa muda wa mwezi mmoja (SIKU 30) tokea tarehe ya taarifa hii.

Endapo offer hii ikionekana irudishwe Manispaa ya Ilemela S.L.P 735, Mwanza.

**Stephen B. Mabana**
**KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA ILEMELA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**
**BARUA ZOTE ZIANDIKWE KWA MKURUGENZI WA MANISPAA**
**SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA**
**Ofisi ya Mkurugenzi,**
**OFISI ZOTE: +255 736 200911/12**
**Manispaa ya Ilemela,**
**FAX:+255 028 736 200910, S.L.P 735,**
**E-mail: Ilemela Municipal@yahoo.com MWANZA**

**Kumb.Na.IMC/L/36725/12/SBM**
**Tarehe: 24/08/2023**
**Kwa yeyote anayehusika,**
**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO (LETTER OF OFFER) YA KUMILIKI ARDHI .**

**Offer ya kiwanja Na. 566 Kitalu 'LL' KILOLELI.**
Mmiliki aliyeandikishwa: **HUSSEIN HASSAN LUGWISA** wa S.L.P 875, Mwanza.

Muombaji: **SHANI HUSSEIN LUGWISA** wa S.L.P 875, Mwanza.

**TAARIFA IMETOLEWA kwamba offer ya mmiliki wa ardhi** iliyotajwa hapo juu imepotea, na ninakusudia kutoa offer mpya badala yake iwapo hakuna pingamizi lolote kwa muda wa mwezi mmoja (SIKU 30) tokea tarehe ya taarifa hii.

Endapo offer hii ikionekana irudishwe Manispaa ya Ilemela S.L.P 735, Mwanza.

**Stephen B. Mabana**
**KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA ILEMELA**

# Zabuni iliyopewa kampuni ya kigeni yafutwa

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imefuta zabuni inayohusu uwekaji alama katika mafuta iliyotolewa kwa Kampuni ya Uswisi, M/S SICPA SA na kuliagiza Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuanza upya mchakato huo.

Mwenyekiti wa mamlaka hiyo, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Sauda Mjasili na wajumbe wawili, Wakili Rosan Mbwambo na Pius Mponzi, walifikia uamuzi huo baada ya kuikubali sehemu ya rufani iliyowasilishwa na kampuni kutoka Marekani, M/S Authentix Inc, ikipinga uamuzi wa TBS kutoa zabuni hiyo kwa M/S SICPA SA.

Katika uamuzi wake iliyoutoa Agosti 11 mwaka huu, mamlaka hiyo iliamua kuwa TBS ilifanya makosa ya kisheria wakati wa tathmini ya zabuni ya usambazaji wa mitungi ya plastiki ya alama za mafuta, jeri za chuma, mfumo wa dozi ya mafuta na mfumo wa kugundua alama za mafuta iliyohusisha kampuni tatu za kimataifa.

Mamlaka ilieleza kuwa SICPA SA haikustahili kushiriki katika mchakato huo kutokana na tuhuma za rushwa inayotuhumiwa.

Baada ya kupitia kumbukumbu za rufani, kamati hiyo ilibaini kuwa Aprili 2 mwaka huu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Uswisi ilitoa amri ya muhtasari wa adhabu kuitaka Kampuni ya SICPA SA kulipa Sh. bilioni 216 kama adhabu kwa ushiriki wa wafanyakazi wake katika vitendo vya rushwa kwa maofisa wa kigeni.

Mamlaka ya Rufani iliona zaidi kwamba SICPA SA haikupinga kuwapa adhabu hiyo, badala yake ilieleza kuwa adhabu hiyo haiwezi kuchukuliwa kama amri ya mahakama au tuzo ya usuluhishi.

Zaidi ya hayo, mamlaka ilipitia Kanuni ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Uswizi na kuona kwamba kifungu cha 354 kinaruhusu mshtakiwa au mtu mwingine yeyote ambaye ameathiriwa na utoaji wa amri ya muhtasari wa adhabu, kuwasilisha pingamizi la maandishi.

Baada ya kupitia kumbukumbu za rufani, mamlaka iliona kuwa Kampuni ya SICPA SA ilikubali amri hiyo na hakuna pingamizi halali lililowasilishwa.

Mamlaka pia ilizingatia pendekezo la Kampuni ya SICPA SA kwamba muhtasari wa amri ya adhabu ulihusiana na uchunguzi uliofanywa kuanzia mwaka 2008, hivyo hauingii ndani ya muda ambao ulitakiwa kubainishwa katika mchakato wa zabuni.

Vilevile, mamlaka ilikataa pendekezo la kampuni hiyo ya Uswisi kwamba amri hiyo ilihusu wafanyakazi na siyo kampuni yenyewe kwa sababu kampuni hiyo inawajibika kwa vitendo vya wafanyakazi wake.

Mamlaka ya Rufani pia ilizingatia malalamiko ya kampuni ya Marekani kwamba TBS ilitoa zabuni hiyo kwa SICPA SA kabla ya kumalizika kwa muda unaotakiwa.

Pia ilibainisha kuwa notisi ya nia ya kutoa zabuni ilitolewa Juni 9 mwaka huu na siku saba za kutoa malalamiko ziliisha Juni 20 mwaka huu. Kwa mujibu wa hukumu hiyo, Juni 16 mwaka huu kabla ya kuisha kwa muda, TBS ilitoa zabuni hiyo kwa Kampuni ya Uswisi, M/S SICPA SA.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Dk. Juma Mhina (wa pili kulia), akizungumza na madiwani jana nje ya mkutano wa Baraza la Mamlaka ya Mji wa Muheza katika ukumbi wa Orofea. Wa tatu kushoto; Diwani wa Kata ya Genge, Moses Kisiki, Diwani wa Majengo, Mukadam Sabuni na kulia ni Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji, Johari Mtango. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# NEEC yataka vijana watumie fursa za kujikwamua kiuchumi

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amewataka vijana nchini kutokata tamaa badala yake wachangamkie fursa mbalimbali za kujikwamua kiuchumi na kubadilisha maisha yao.

Akizungumza pembezoni mwa kongamano lililowakutanisha wakurugenzi mabinti ambao wamefanikiwa katika biashara kutoka taasisi mbalimbali jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Issa aliwapongeza vijana hao kwa hatua walizofikia kwa sababu mafanikio hayo yatakuwa chachu kwa vijana wengine kuiga mfano huo.

"Vijana hampaswi kukata tamaa mkizingatia kuwa serikali imeanzisha programu mbalimbali ya kuwainua vijana na wanawake ikiwamo Jenga Kesho iliyo Bora au 'Build a Better Tomorrow' (BBT). Mpango huu unalenga kuwavutia vijana wengi kuwekeza kwenye kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwa sekta hizo zina fursa nyingi zinazoweza kubadilisha maisha yao," alisema.

Aliongeza kuwa baraza kama nguzo muhimu ya kuwaunganisha vijana, wanawake na Watanzania kwa ujumla, litaendelea kutoa elimu na kuwahamasisha kuchangamkia fursa kwa kuwekeza katika biashara ikiwamo kilimo, mifugo, uvuvi na kujenga kizazi chenye nguvu na mshikamano cha vijana katika biashara na uongozi nchini.

"Lengo la kongamano hili ni kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto, kubalilishana uzoefu, kutambua fursa zilizopo katika uwekezaji sambamba na kubadilishana ujuzi na maarifa ili kujikwamua kiuchumi na hivyo kutoa mchango stahiki katika kukuza Pato la Taifa," alisema Issa.

Alisema kundi la viongozi wa kike kupitia kongamano limeonyesha lina uwezo wa kuthubutu kufanya mambo ambayo wengine hawawezi kuyafanya katika biashara na hivyo kutupa uhakika kuwa miaka 10 ijayo nchi itakuwa na wafanyabiashara wakubwa kwa kuwa biashara ni mchakato, inamwitaji mtu mwenye uvumilivu, mwajibikaji na asiyekata tamaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Young CEO Foundation Roundtable, Zakayo Shushu, mbali na kuainisha malengo ya taasisi yake, alisema wamejipanga kuwafikia vijana wengi zaidi ambao wako tayari kuzifanyia kazi ndoto zao ikiwamo ya kujiajiri licha ya kuwapo changamoto nyingi katika hatua wanazozipiga.

"Sisi kama taasisi tumeendelea kujipambanua na kuhakikisha vijana wa Tanzania hususani mabinti wanashiriki vyema katika kutoa mchango stahiki katika kukuza Pato la Taifa, ndiyo maana ya kongamano hili," alisema Shushu.

## TCRA na COSTECH waungana kuwezesha kampuni zinazochipukia

**Na Frank Monyo**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) pamoja na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) zimeungana kwa lengo la kutoa rasilimali za mawasiliano bila malipo kwa kampuni zinazochipukia katika sekta ya teknolojia za kidijiti.

Hatua hiyo inalenga kuweka mazingira bora ya kuvutia uvumbuzi wa kidijiti nchini na kuhakikisha kampuni hizo zina nafasi ya kukua na kufanikiwa.

Mwishoni mwa wiki mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisisitiza mpango huo unalenga kuwapa vijana wabunifu zana wanazohitaji kwa majaribio ya huduma zao kwa kipindi maalum.

Alisema hadi kufikia Juni mwaka huu, TCRA ilikuwa tayari imetoa rasilimali hizo muhimu kwa kampuni nne, huku akiwahimiza wajasiriamali vijana, wabunifu na watafiti kuwasilisha mawazo yao ya kibunifu kwa COSTECH na kuwahakikishia kwamba baada ya idhini kutoka COSTECH, watapata rasilimali hizo bila gharama yoyote.

Alisema rasilimali za mawasiliano ni msingi wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano, kama vile huduma za fedha za simu na huduma nyingine zinazotegemea teknolojia za kidijitali kama vile kilimo cha kisasa, biashara mtandao, usafirishaji, uendeshaji wa taasisi binafsi.

"Hapo awali, ili uweze kujaribu kitu chochote katika anga la mtandao, ilibidi upate leseni na kutoa gharama kubwa.

"Sasa tunasema kama wewe ni mwanafunzi au mbunifu umeingia kwenye ulimwengu wa kidijiti, umegundua kitu na umetengeneza kitu kinachoweza kuleta manufaa makubwa, na unataka kukijaribu na katika kukijaribu unahitaji rasilimali kama namba, masafa, au hata kushirikiana na kampuni za simu; tunasema majaribio kama hayo ni bure.

"Ugawaji wa rasilimali hizi unawezesha huduma za mtandao zenye kasi kubwa, jambo ambalo ni muhimu katika uchumi wa kidigitali. Wabunifu wenye ubunifu unaoleta suluhu kwa changamoto za jamii, sasa wataweza kushirikiana na TCRA, COSTECH na watoa huduma hasa mitandao ya simu ili kubeba ubunifu huo," alisema.

Dk. Bakari alizitaja miongoni mwa rasilimali zinazotolewa na TCRA ni rasilimali-namba (numbering resources), masafa (frequency spectrum), postikodi na anwani za makazi.

Meneja wa Chama cha Wabunifu, Tanzania Start-Ups Association (TSA), Praygod Japhet, akizungumzia mpango huo, alisema kuwa awali rasilimali hizo za mawasiliano zilipatikana kwa gharama kubwa, mara nyingi hadi kufikia Sh. milioni 10 kulingana na huduma, lakini sasa kwa ushirikiano wa TCRA na COSTECH, wabunifu chipukizi wanapata rasilimali hizo bila malipo.

"Hii imesaidia kupunguza mzigo kwa wabunifu wengi, ambao mara nyingi ni vijana kutoka vyuo vya kati na vikuu na ambao wamekabiliana na changamoto za upatikanaji wa mitaji.

"Hatua hii inaleta rasilimali adimu na za gharama kwa wabunifu, ambazo zitasaidia kuboresha jamii ya Watanzania," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Habari wa COSTECH, Mary Kigosi, alisema ushirikiano kati ya taasisi yao na TCRA umesaidia kupunguza changamoto kwa wabunifu wa teknolojia ya kidijiti ambao awali walikuwa wanakabiliana na changamoto ya kupata zana hizo muhimu kwa maendeleo yao.

TANGAZO

# GBT yajizatiti mapambano dhidi ya mashine haramu za sloti 'Dubu'

**Mwandishi wetu**

Baada ya kuonekana kuwa sekta ya michezo ya kubahatisha ina tija, Serikali iliunda Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) mnamo mwaka 2003 kwa lengo la kuhakikisha Tanzania inanufaika kiuchumi pasi na kuleta madhara katika jamii ya Watanzania.

Chini ya usimamizi wa GBT, Serikali na jamii imepata mafanikio lukuki ikiwemo kuongezeka kwa mapato mwaka hadi mwaka na kuchochea maendeleo katika utoaji wa huduma na michezo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha(GBT), James Mbalwe, katika mwaka wa fedha 2021/22, mapato yatokanayo na kodi kutoka katika sekta hiyo yaliongezeka na kufikia Sh bilioni 148.

Mapato hayo yameongezeka zaidi katika mwaka wa fedha uliofuata yaani 2022/23 ambapo takwimu zinaonesha kuwa kuwa yaliongezeka na kufika kiasi cha Sh bilioni 170.43

Mbali na mapato hayo kwa njia ya kodi, bado sekta ya michezo ya kubahatisha inatoa ajira kwa Watanzania. Mkurugenzi huyo anaeleza kuwa suala la ajira ni moja ya mahitaji makubwa kwa Serikali. Takwimu za karibuni zinaonesha kuwa takribani watu 25,000 wamenufaika na ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja katika sekta.

"Kama kuna watu 25,000 na walioko nyuma yao wanawategemea unaweza kuona ni kwa kiasi gani sekta hii ilivyo na mchango mkubwa katika nchi," anasema Mkurugenzi wa GBT, James Mbalwe.

**Kuendeleza Michezo na sekta nyingine**

Sheria iliyopitishwa na Bunge mnamo mwaka 2019 iliweka bayana kuwa asilimia 5 ya kodi inayopatikana kutokana na michezo ya ubashiri itaenda Baraza la Michezo la Taifa (BMT) lililopo chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kusaidia kukuza michezo kama soka, riadha, kikapu, ngumi na michezo mingine.

Mbali na uwepo wa Sheria hiyo, Mkurugenzi wa GBT anasema waendeshaji wa michezo ya kubahatisha wanasaidia maendelo ya michezo kupitia udhamini wa vilabu na hivyo kuifanya ligi kuwa bora na yenye ushindani kwa hapa ndani na hata kwa nje ya nchi.

"Ligi yetu imeimarika sana...vilabu vyetu vimefanya vizuri nasikia Ligi ya Tanzania ni ya tano kwa ubora katika Bara la Afrika. Kuna mchango mkubwa sana wa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha," anaeleza.

Hata hivyo, sekta hii haijaacha nyuma katika kusaidia sekta nyingine kama elimu, maji na afya kutokana na fedha zinazopatikana kuwekezwa kwenye maeneo hayo ili kuinua ustawi wa Mtanzania. Katika hili, Mkurugenzi Mbalwe anasema: "Kwa ufupi niseme tu kwamba sekta hii imekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi."

**Changamoto ya mashine za sloti/dubu**

Pamoja na mafanikio makubwa, sekta hii inapitia changamoto moja kubwa, ambapo hivi karibuni kumezuka tabia ya wananchi kuweka mashine za sloti maarufu dubu au dumbwi kiholela huko mitaani. Jambo ambalo limeleta kero kwa jamii na kuharibu taswira ya sekta ya michezo ya kubahatisha nchini.

"GBT haiwezi kuacha hali hii iendelee na kuifanya sekta kuwa ni sehemu ya watu kufanya jinai." alisema Mkurugenzi Mbalwe na kuongeza kuwa "kwa kuzingatia hali hiyo, GBT imekuja na kampeni kubwa dhidi ya waendeshaji wote haramu wa biashara ya mashine za sloti inayoitwa "FICHUA, Tukomeshe Mashine Haramu; Ukiziona Tuonyeshe".



*Mashine haramu za sloti maarufu kama 'dubu' zilizokamatwa katika maeneo mbalimbali zikiteketezwa huko Kisarawe mkoani Pwani hivi karibuni.*

Mbalwe alisisitiza kuwa "Sekta ya michezo ya kubahatisha isiposimamiwa vema, inaweza kuwa na madhara makubwa katika jamii. Hata hivyo, GBT imejizatiti kuisimamia sekta hiyo kuhakikisha kuwa michezo hiyo inakuwa salama na si kichaka cha jinai,"

Hata hivyo, uwepo wa waendesha haramu hasa wa mashine za sloti ama maarufu mashine za dubu, unatokana na baadhi ya watu wasio waaminifu kutumia mwanya wa kushamiri kwa biashara hiyo kuendesha biashara hiyo kinyume cha utaratibu na Sheria. Moja ya ukiukwaji wa taratibu hizo ni pamoja na kuingiza mashine hizo bila kufuata taratibu. Vile vile kuendesha biashara hiyo katika maeneo yasiyosajiliwa na pia mashine kuwekwa holela kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kama kwenye Salon, dukani 'kwa mangi', kwa mama ntilie au katika makazi ya watu kwenye nyumba zisizo za kibiashara.

Licha ya mashine hizo kutotambuliwa katika mifumo ya GBT, waendeshaji hao haramu wamekuwa wakihusisha watoto chini ya miaka 18 ambao kisheria hawaruhusiwi kushiriki kwenye michezo ya kubahatisha jambo ambalo linaharibu taswira nzima ya sekta ya michezo ya kubahatisha.

**Utambuzi wa mashine haramu**

Mashine za sloti/dubu kisheria zinaruhusiwa kuwekwa katika maeneo mawili tu; kwenye baa na maduka maalum yam ashine hizo (Slot Shops).

Tofauti na maeneo hayo, biashara hiyo itakuwa ni HARAMU na inaendeshwa kinyume cha Sheria. Pamoja na kuwekwa kwenye eneo linaloruhusiwa, ni lazima pia eneo husika liwe na leseni iliyo hai (Valid License).

"Wanaoendesha biashara ya mashine za sloti zisizokuwa na usajili (HARAMU) wanaweza kubainika kwani hawana leseni hai ya biashara na vibali vya kufanyia biashara mahali ilipo mashine kwa wakati huo na stika maalum za Bodi ya Michezo ya Kuhabatisha (GBT)," alifafanua Mkurugenzi Mbalwe.

Aidha, Mkurugenzi wa GBT amewasihi wananchi kuwa endapo wakiona wamiliki wa mashine za sloti wakiendesha shughuli zao bila ya vibali au kuchezesha katika maeneo yasiyoruhusiwa na kuruhusu watoto kucheza, basi watoe taarifa GBT kwa kupiga simu ya bure 0800 11 00 51 au kupitia barua pepe: **info@gamingboard.go.tz** au kwenye kituo cha Polisi kilichopo karibu.

Mkurugenzi Mbalwe ameongeza kuwa, kuna baadhi ya watu wamekuwa wakitumia majina ya kampuni zilizosajiliwa kuendesha biashara kinyume cha Sheria. Hivyo kuwashauri wananchi kupiga simu za kampuni husika kupata uhakika kwani kuna wengine huendeshea shughuli hizo sehemu zisizosajiliwa.

Donge nono litatolewa kwa mwananchi yeyote atakayetoa taarifa za kweli na uhakika zitakazowezesha kukamatwa kwa wahalifu wanaoendesha biashara ya mashine za sloti/dubu/dumbwi au kuziingiza nchini au kuzitengeneza bila ya leseni, kibali au idhini kutoka GBT.

GBT inawataka wale wote wanaoendesha biashara ya mashine hizo huko mitaani kiholela bila kuwa na leseni kuacha kufanya hivyo mara moja. Adhabu ya kifungo kisichopungua miezi 12 au faini ya shilingi milioni moja au vyote kwa pamoja vitatolewa kwa watakaokutwa na kosa hilo

Mbali na hatua hiyo, GBT imejizatiti kuhakikisha kuwa inawekeza katika teknolojia ili kubaini vitendo vya kihalifu katika sekta hiyo ili ibaki katika dhamira ya kuwepo kwake na kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi.

**Wito kwa jamii**

Kukabiliana na mashine haramu za sloti ama dubu mitaani ni jambo linalohitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali, anasema Mkurugenzi wa GBT."Hivyo ni muhimu kupata ushirikiano kwanza kabisa kutoka kwa Serikali na wananchi," anasema Mkurugenzi huyo wa GBT.

Ameongeza kuwa iwapo jamii itashikamana katika mapambano dhidi ya mashine haramu za sloti au uvunjifu mwingine wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo, na wachezaji wakaelewa dhana nzima ya michezo ya kubahatisha kuwa ni burudani wala siyo kazi au chanzo cha pesa, Taifa litanufaika kupitia michezo hiyo kwa mapato na kuinua maisha ya mwananchi kupitia huduma kadhaa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga msibweteke, raundi ya kwanza ngumu

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Yanga wameungana na watani wao wa jadi, Simba kutinga raundi ya kwanza kuwania kufuzu hatua ya makundi.

Yanga iliyoanzia hatua ya awali imeungana na Simba, ambayo ni miongoni mwa klabu nane bora Afrika zinazoanzia raundi ya kwanza ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu.

Katika raundi ya awali, Yanga imesonga mbele baada ya kuitoa ASAS FC ya Djibouti kwa jumla ya mabao 7-1, ikishinda mechi ya awali (ugenini) mabao 2-0 kabla ya mchezo wa marudiano nyumbani kushinda 5-1.

Hata hivyo, mechi zote mbili zilichezwa hapa nchini, baada ya ASAS kuomba kuutumia Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam kama wao wa nyumbani kutokana na viwanja vyao kutokukidhi vigezo vya CAF.

Kwa kutinga hatua hiyo sasa Yanga inakwenda kukutana na Al-Merrikh ya Sudan ambayo imeitoa AS Otoho d'Oyo ya Congo kwa faida ya bao la ugenini baada ya mechi ya ugenini kutoka sare ya bao 1-1 huku nyumbani zikitoka suluhu.

Kwa Simba itakutana na Power Dynamos ya Zambia ambayo nayo imetinga hatua hiyo kwa faida ya bao la ugenini baada ya mechi ya ugenini kufungwa mabao 2-1 na nyumbani kushinda 1-0 dhidi ya African Stars ya Namibia.

Kwa ujumla hizi si mechi rahisi kwa wawakilishi wetu hao, kwani hapa ndipo hatua ngumu na muhimu ya michuano hiyo inapoanzia, kwa kuwa kila timu inahitaji kutinga hatua ya makundi ili kuanza kunufaika na dau linalotolewa na CAF.

Ikumbukwe hatua ya makundi timu mbili zitakazoongoza kila kundi zitatinga robo fainali, lakini hata itakayoburuza mkia kwenye kila kundi zote zitaondoka na donge nono.


Kwa Yanga haina budi kutambua inaenda kukutana na timu ya daraja la juu zaidi na si kama ASAS FC ambayo imecheza mechi zake za nyumbani hapa nchini, lakini ikumbuke ilipojikwaa msimu uliopita baada ya kutolewa katika hatua hiyo na mahasimu wakubwa wa Al Merrikh, Al Hilal ya Sudan.

Licha ya kwamba Al-Merrikh inacheza mechi zake za nyumbani nchini Rwanda kutokana na machafuko ya kisiasa nchini Sudan, hilo pia halitoshi kuifanya Yanga kubweteka, bali kufanya maandalizi makubwa ili kutinga hatua hiyo ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika waliyoikosa kwa zaidi ya miaka 20.

Kwa upande wa Simba, pia pamoja na kuwa na uzoefu mkubwa katika michuano hiyo kwa kufika hatua ya makundi, haina budi pia kujipanga vema dhidi ya Power Dynamos ambayo waliifunga kwenye mechi ya kirafiki ya Simba Day mabao 2-0.

Tunatambua hii itakuwa ni mechi tofauti na wapinzani wao hao tayari wanajua uchezaji wa Simba, hivyo watakuja kivingine nao wakitamani kutinga hatua ya 'neema', makundi Afrika, hivyo tunawatakia wawakilishi wetu hao maandalizi mema kwani lengo letu ni kuona msimu huu zikifika nusu fainali hata kucheza zenyewe fainali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Azam kuna tatizo zito hapa hata kuliko inavyodhaniwa

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza nimeona mashabiki wa Azam FC wakilia na kulalamika kuhusu timu yao. Kumbe ina mashabiki wenye uchungu na timu hiyo ingawa si idadi kubwa kama ile ya Klabu za Simba na Yanga.

Ijumaa iliyopita baada ya kutolewa kwenye hatua za awali za Kombe la Shirikisho barani Afrika, walikuja juu na kutapika 'nyongo'.

Mashabiki wa Azam ambao kwa kawaida huwa ni wapole na hupokea matokeo yoyote ya timu yao, kawaida tu, 'waliliamsha' na kutaka uongozi uwajibike kwa kile kilichotokea siku hiyo katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ilipotolewa dhidi ya timu kutoka Ethiopia, Bahir, Dar Kenema kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Licha ya kushinda mabao 2-1, lakini penalti zilihusika kwa sababu katika mechi ya kwanza ilifungwa ugenini mabao 2-1, hivyo matokeo ya jumla yakawa 3-3. Azam ilikosa penalti tatu, wenzao mbili, hivyo kusonga mbele kwenye hatua ya raundi ya kwanza ya michuano hiyo ya kimataifa.

Ni kama marudio tu ya msimu uliopita ilipotupwa nje ya michuano hiyo raundi ya kwanza dhidi ya Al Akhdar ya Algeria, ilifungwa ugenini mabao 3-0, lakini ilishindwa kupindua meza nyumbani licha ya ushindi wa mabao 2-0, hivyo kuondolewa kwa jumla ya mabao 3-2.

Kuhusu suala la usajili hakuna msimu ambao Azam haijasajili wachezaji wazuri. Ina wachezaji ambao hata wakisajiliwa na Klabu za Simba na Yanga wanakwenda kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza.

Mashabiki wengi wa soka nchini wanashangaa kwa nini wanakosa muunganiko kwenye kikosi cha Azam na kufanya vizuri? Kuna eneo lina tatizo.

Makipa wengi wanaosajiliwa kwenye kikosi hiko huwa ni wazuri na bora wanakotoka, na hata wanapocheza mechi za kwanza za timu hiyo mashabiki wanashuhudia ubora wao, lakini kadri muda unavyozidi kwenda wanaanza kuwa na makosa mengi na viwango vyao kushuka.

Imekuwa ikielezwa kuwa Azam huwa haitendewi haki na waamuzi katika baadhi ya mechi kwenye Ligi Kuu, hivyo haikataliwi, lakini mbona kwenye mechi za kimataifa ambako marefa wanachezesha haki pia haifanyi vizuri? Kuna tatizo mahala.

Inakuwaje Azam FC iliyoanza kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2008/09 na kuwa na uwekezaji mkubwa, ikiwa haina uhaba wa pesa haijawahi kucheza hatua ya makundi hata ya Kombe la Shirikisho, achilia mbali ya Ligi ya Mabingwa? Kuna tatizo sehemu.

Kuhusu Kocha Youssouph Dabo kwangu binafsi hata kama atafukuzwa sioni kama ndiyo sababu yeye kupoteza kwa sababu miaka ya nyuma hakuwapo na ilikuwa haifuzu pia.

Kumfukuza Dabo wala si dawa kwa sababu Azam ni moja kati ya timu iliyofukuza makocha wengi wakiwamo, Mohamed King, Neider Santos, Itamar Amorin, Stewart Hall, Boris, Bunjak, Joseph Omog, George Nsembe, Zeben Hernanderz, Aristica Cioaba, Hans van Pluijm, Abdul Mingange, Etienne Ndayiragije, George Lwandamina na Abdihamimd Moallin, lakini kwa miaka yote hi haijawa dawa ya kufanya vizuri.

Ni wakati sasa wa kuanza kutazama juu, siyo kwa wachezaji na makocha ambako kuna wachezaji wazuri na makocha wengi wanaokuja wamefanya vema walikotoka.

Wamiliki, kama itawapendeza ni wakati wa kufumua uongozi mzima na mfumo wote na kutengeneza upya. Hata ikiwa ni lazima kuwapata viongozi kama Ofisa Mtendaji Mkuu toka nje ya nchi sawa tu.

Kama wamiliki wanataka Azam iwe ipo ipo tu sawa, ila watawapoteza mashabiki wao hata wao wachache walionao, lakini kama wanataka iendelee kuzoa mashabiki ni lazima ifumue uongozi mzima.

# HABARI KITAIFA

## LHRC yatoa angalizo kanuni Sheria ya Habari

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, ameshauri Kanuni za Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ambazo ziko mbioni kutungwa, zipoze suala la makosa ya kiuandishi wa habari kuitwa uchochezi.

Dk. Anna alitoa angalizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha siku moja cha Wadau wa Haki ya Kupata Habari (CoRI) kilichoitishwa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Kikao hicho kililenga kupitia vipengele vya Sheria ya Huduma za Habari vilivyopitishwa na Bunge mwaka huu, pia kuangalia mwelekeo wa Kanuni za Sheria ya Habari ambazo ziko mbioni kutungwa.

"Sera ya Habari inayokuja, ipooze hili suala la waandishi wa habari kuitwa wachochezi. Iondoe yale makosa ya jinai kwa kuwa suala la kupashana habari halipaswi kuwa na jinai ndani yake," alishauri.

Dk. Anna alisema suala la kupashana habari ni haki ya kikatiba, makosa yanaweza kutoka kama ilivyo kwa mwanadamu yeyote, hivyo kufanya makosa hayo ya kitaaluma kuwa jinai, ni kuifinya tasnia ya habari.

"Katiba yetu Ibara ya 18 inasema "...mtu ana haki ya kutoa, kupokea na kupata habari". Kanuni zitu zizibe ile mianya inayomtia shaka mwanahabari," alisema.

Dk. Anna pia alishauri serikali kuendelea kutengeneza mazingira mazuri kwa waandishi wa habari kama ilivyo nia ya Rais Samia Suluhu Hassan. Inawezekana sheria kurejeshwa bungeni kufanyiwa marekebisho hata kama haijaanza kutumika.

"Wito wangu, sheria haikatazi kufanya mabadiliko ya sheria mara kwa mara. Kwa kuwa sheria ya habari bado ina kasoro, inaweza kupelekwa tena bungeni na kurekebishwa," alishauri.

Naye Dk. Darius Mukiza kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano kwa Umma (SMJC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alishauri kuwe na mafunzo kuhusu sheria ya habari katika vyuo vinavyotoa taaluma hiyo.

"Mambo yote kuhusu Sheria ya Habari yanapaswa kuingizwa katika vyuo vya habari. Vijana wanatoka vyuoni wakiwa hawajui chochote kuhusu sheria hizi," alisema Dk. Mukiza.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji TEF, Neville Meena, alisema waandishi wa habari wasio na sifa ya elimu inayohitajika katika tasnia ya habari, wanapaswa kushinikizwa kufanya hivyo kwa kuwa fursa ipo.

"Tutakuwa watu wa ajabu kama tutaendelea kukumbatia watu wasio na sifa katika tasnia ya habari. Fursa ipo, tuwahimize ili wawe na sifa," alisema Meena.

Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA - TAN), James Marenga, alisema hatua ya Bodi ya Ithibati kusimamiwa na serikali, inanyima uhuru waandishi wa habari kujisimamia.

"Bodi ya Ithibati wajumbe wake wanateuliwa na waziri, inasimamiwa na waziri kwa maana ya serikali na ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia waandishi na hata kuwanyang'anya leseni. Hili linanyima uhuru waandishi wa habari," alisema Marenga.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema mchakato wa kutunga kanuni za habari unakaribia kuiva, hivyo akaishauri serikali kukutana na wadau wa habari na kupitia kanuni hizo kabla ya kuanza kutumika.



Mkuu wa Idara ya Biashara na Huduma za Serikali wa Benki ya NMB, Vicky Bishubo (kulia), akimkabidhi vifaa mbalimbali Mkurugenzi wa Kituo cha New Hope for Girls, Dk. Consoler Eliya (kushoto), vilivyotolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, ikiwa ni msaada kwa kituo hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waziri Mchengerwa akaribisha wawekezaji Rufiji

**Na Mwandishi Wetu,**
RUFIJI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohammed Mchengerwa, amewakaribisha wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania kuwekeza katika fursa zilizoko wilayani Rufiji mkoani Pwani.

Mchengerwa amesema Rufiji ambayo ni kati ya wilaya kongwe nchini, inazidi kukua kila siku kwa kuimarisha miundombinu ya huduma za jamii kwa kuwa tayari serikali imejenga zahanati 24, shule za msingi 45 na sekondari tisa ndani ya vijiji 38 ilivyonavyo zinazotoa nafasi kwa wananchi kutibiwa na watoto kupata elimu itakayowasaidia kujikomboa katika maisha yao.

"Uamuzi wa serikali kujenga Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) umeleta neema nyingi zitakazowanufaisha wananchi na halmashauri hiyo yenye utajiri mkubwa wa ardhi, maliasili na utamaduni.

"Ukiacha bwawa hili, kuna hekta 300,000 zimetengwa kwa ajili ya kilimo kitakachoendeshwa kwa mfumo wa umwagiliaji. Ni wakati sahihi sasa kwa wawekezaji kutoka ndani na nje ya Tanzania kuja kuwekeza wilayani Rufiji kwa kuwa kuna usalama wa kutosha kuanzia namna ya kuhifadhi fedha zao mpaka kutekeleza miradi watakayoianzisha," alisema Mchengerwa wakati wa uzinduzi wa wa tawi Benki ya CRDB huko Ikwiriri, wilayani Rufiji.

Ili kutoachwa nyuma, Mchengerwa ambaye pia ni Mbunge wa Rufiji, tangu mwaka 2015 amewahimiza wananchi wenzake kulitumia tawi hilo la benki, hivyo kunufaika na huduma zinazotolewa na kujihakikishia usalama wa fedha, kukopa kwa ajili ya miradi na mipango binafsi hata kufanya uwekezaji.

"Rufiji ni kati ya wilaya kongwe nchini, lakini kwa muda mrefu haikuwa imefunguka ila leo (Agosti 25 mwaka huu) benki hii imeonyesha njia. Ili kuwa wilaya ya sita wakati wa mkoloni na ya 13 baada ya uhuru.

"Mimi ni mteja wa siku nyingi wa benki hii, hivyo nawasihi wananchi wenzangu nanyi mjiunge kutumia huduma zao. Benki hii inayo huduma ya Imbeju ambayo ni programu maalum ya kuwawezesha vijana na wanawake. Makundi haya muhimu kwa jamii yetu, yapo wilayani Rufiji na kwa kufika kwenye tawi hili ndivyo yatakavyoweza kunufaika na programu hii inayotoa mtaji wezeshi kwao.

"Kwa kuwa Rufiji ina kila kitu kinachohitajika kwa mjasiriamali kujikwamua kiuchumi, mtaji huu unaotolewa na benki hii na mikopo ya aina tofauti iliyopo ni msingi mkubwa wa kuwakomboa wananchi kiuchumi," alisema Mchengerwa.

Waziri huyo alizitaja fursa nyingine zilizoko wilayani mwake ni pamoja na kilomita za mraba 6,500 ambazo ni hifadhi na misitu zinazofaa kwa utalii.

Fursa nyingine kwa mujibu waziri huyo ni uvuvi, huduma za kijamii na ukarimu zikiwamo hoteli. Kwenye kilimo, Mchengerwa alisema ufuta, korosho na mazao mengine mengi ya biashara yanastawi vyema wilayani Rufiji na hivi karibuni kiwanda kikubwa cha sukari kitajengwa huko.

Kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema wamejipanga vyema kukidhi mahitaji ya mtaji kwa ajili ya wateja wao wakiwamo wawekezaji wanaohitaji Shilingi na fedha za kigeni.

"Jana (Agosti 24 mwaka huu) benki yetu imepata kibali za kuorodhesha hatifungani ya kijani yenye thamani ya Dola milioni 300 za Marekani ambazo ni sawa na Sh. bilioni 780.

"Fedha zitakazokusanywa kutokana na mauzo ya hatifungani hii zitaelekezwa katika miradi inayolinda na kujali mazingira. Rufiji ni kati ya maeneo yanayostahili kuzitumia, hivyo ninawakaribisha mje tuwape huduma," alisema Raballa.

Ofisa huyo alisema kuwa kupitia tawi hilo, wananchi wa wilaya nzima ya Rufiji wanafunguliwa milango kunufaika na mtandao mpana wa matawi 260 yanayoifanya benki hiyo kuwa na idadi kubwa zaidi kulinganishwa na benki nyingine nchini.

Mbali na huduma katika matawini, ofisa huyo alisema kupitia mawakala wa benki, mashine za kutolea fedha na zile zinazopokea malipo ya kadi au kupitia simu ya mkononi, benki hiyo pia inatoa ushauri na elimu kuhusu masuala ya fedha, uwekezaji na namna bora ya uendeshaji wa biashara.


"Watu wengi hudhani benki ni kuweka, kutoa fedha au kuomba mkopo tu. Ukweli wasioujua ni kuwa tunatoa elimu na ushauri na tumekuwa tunafanya hivyo kwa wateja wetu ingawa wengi hawaitumii huduma hii.

"Hivyo niwakaribishe katika benki yenu kupata ushauri. Tunafanya uwezeshaji kwa wanawake na vijana kwa kuwapa mitaji wezeshi kwa masharti nafuu ili kuwapa nafasi ya kuimarisha kipato chao na kushiriki kujenga uchumi wa taifa," alisema Raballa.

Benki hiyo ndiyo taasisi pekee ya kizalendo yenye matawi nje ya mipaka ya Tanzania, ikitoa huduma Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**





Mchuuzi wa machungwa katika Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam, akiyapanga kwenye eneo lake la biashara jana ambapo chungwa moja liliuzwa kwa Sh. 50 kwa bei ya jumla jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanaume wanahitaji elimu kujua viashiria hatarishi kwa wajawazito

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema bado kuna haja kwa wanaume wakiwamo vijana rika balehe kupewa elimu ya afya uzazi ikiwamo suala la uzazi wa mpango ili wajue viashiria vyote hatarishi vinavyoweza kuwapata wajawazito na kuwasaidia kufika haraka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Kaimu Mratibu wa afya ya uzazi kutoka TAMISEMI, Dk. Dastan Mshana, alisema hayo alipokuwa akizungumza na makatibu afya wa wilaya, wafamasia na waratibu wa huduma za mama, baba na mtoto kutoka mikoa minane nchini waliokuwa wakijengewa uwezo wa huduma zinazotolewa kwa wananchi katika mafunzo yaliyotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la utetezi wa masuala ya uzazi, Tanzania Men as Equal Partner in Development (TMEPiD).

Dk. Mshana alisema vijana wa rika balehe pamoja na wanaume bado wanahitaji elimu ya afya ya uzazi na eneo hilo halijapewa msukumo mzuri wa kutosha.

"Kama tutafanya vizuri kwenye eneo hili, tutakuwa na kizazi bora sana cha baadaye, maana vifo vingi vya mama na mtoto vinavyotokea hapa nchini vinasababishwa na ukosefu wa elimu ya uzazi salama, mwanaume au kijana akishajua viashiria vya hatari, hataweza kumuacha mjamzito nyumbani na kuendelea na shughuli zake, lazima atasaidia kumuwahisha hospitali," alisema Dk. Mshana.

Aliwashauri wadau mbalimbali wakiwamo watoa huduma za afya kuendelea kutoa mafunzo zaidi ya afya ya uzazi ikiwamo uzazi wa mpango hususani kwa watu walio pembezoni hasa vijijini ili waweze kujiepusha na changamoto zinazosababisha ongezeko la vifo. Aliwataka kutumia vyema fursa zinazoendelea kutolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha na kujenga miundombinu ya kutolea huduma za afya, ikiwamo ujenzi wa hospitali, vituo vya afya, zahanati pamoja na upatikanaji wa wataalamu na vifaa tiba katika maeneo hayo, kwa kuboresha zaidi huduma na kuhimiza uzazi wa mpango.

"Muhimu sasa ni ninyi kuwa kiungo kizuri kati ya wananchi na serikali baada ya ujenzi na uboreshaji wa vituo vyakutolea huduma, ni vizuri mkajua malengo ya serikali na mikataba mbalimbali ambayo serikali imeingia na muweke kipaumbele ushiriki wa vijana kwenye ajenda ya afya kila jambo," alisisitiza.

Aliwashauri wanaume kujenga tabia ya kwenda kliniki kupata elimu ya uzazi pamoja na wake zao na watoa huduma wasitumie vibaya mpango huo mzuri wa serikali kwa kuwanyima huduma wanawake wanaokwenda peke yao kupata huduma au kuomba rushwa.

Mkurugenzi wa TMEPiD, walioandaa mafunzo hayo, Cuthbert Maendaenda, alisema mafunzo hayo yamelenga kusaidia kuwanusuru wananchi na janga ya afya ya uzazi.

"Makatibu wa afya na mafamasia ndiyo watendaji wakuu watakaoweza kuwasaidia wananchi kwani dawa na vifaa tiba kwenye eneo la uzazi zinahitaji kuhifadhiwa vizuri, lakini zuri linalofanyika juu lazima lianze na msingi mzuri wa mahitaji ya kitaifa huanzia chini, lazima mfahamu utekelezaji wa malengo, mahitaji na wajibu wenu ili kuwa na lugha moja," alisema Maendaenda.

Kaimu Mratibu wa Uzazi wa Mpango Taifa, Getrude Naftali, alisema suala la uzazi wa mpango linatakiwa kupewa kipaumbele katika halmashauri zote nchini ili wananchi wafahamu na kutambua umuhimu wa uzazi salama.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Shamshi Abdalah, ambaye ni Katibu wa afya Halmashauri ya Wilaya ya Chato mkoani Geita, alisema mafunzo hayo yanatarajiwa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya afya.

Mafunzo hayo yameshirikisha makatibu wa afya, wafamasia na waratibu wa afya ya mama, baba na mtoto kutoka halmashauri 16 za wilaya katika mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Mara, Kigoma, Geita, Dodoma na Dar es Salaam ambayo inafadhiliwa katika maeneo mbalimbali ya sekta ya afya na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

# Miaka 21 jela kukutwa na nyara za milioni 7.1/-

**Na Halima Ikunji,** TABORA

FURAHA Seneti (52) mkazi wa Kijiji cha Mpandamlooka, Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, amehukumiwa kifungo cha miaka 21 jela baada ya kukutwa na hatia ya nyara za serikali zenye thamani ya Sh. 7,106,790.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tabora, Demetrio Nyakunga.

Alisema, mshtakiwa huyo alikutwa na makosa manane ya kukutwa na nyara za serikali ambazo ni fuvu la mnyama insha, pembe la parahara, fuvu la tumbili, silaha mbili, risasi kinyume na sheria na taratibu za nchi.

Kadhalika, alisema kesi hiyo imeangukia kwenye makosa ya Uhujumu Uchumi na kosa la nne na la tano kifungu cha 20 (1) (2) cha sheria ya silaha na mlipuko, kosa la saba na nane ni kulipa faini ya Shilingi milioni tano.

Hakimu Nyakunga alisema yanaangukia katika kifungo cha miaka 21 jela baada ya kujiridhisha na ushahidi wa pande zote mbili na mshtakiwa kukiri kutenda makosa hayo.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili, Merito Ukongoji, Nurdin Mmari na Olesta Kemilembi, ulidai kuwa mshtakiwa alikutwa na nyara hizo Septemba 6, 2022 katika Kijiji cha Mpandamlooka saa sita mchana nyumbani kwake.

Mshtakiwa Seneti aliiomba mahakama hiyo impunguzie adhabu kutokana na kuwa na familia inayomtegemea na mama yake mzazi ambaye ni kikongwe akiwa ni mlezi wa familia yake.

Licha ya utetezi huo mahakama iliutupilia mbali kwa kile kilichoelezwa kuwa adhabu hiyo ni kwaajili ya kutoa fundisho kwa wote wanaojihusisha na mauaji ya wanyamapori na kumiliki nyara za serikali kinyume na taratibu za nchi.

# Tanzania yahimiza mikakati kukuza biashara mtandao

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imezitaka taasisi za Posta Afrika kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali kwenye shughuli zote ili kuendeleza biashara mtandao na kufikisha huduma zaidi za kifedha kwa jamii.

Akifungua mikutano ya kamati mbalimbali za Umoja wa Posta Afrika (PAPU) inayoendelea jijini Arusha, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele, alisema matumizi ya TEHAMA yataongeza kasi, ubora na ufanisi wa huduma za posta barani Afrika.

Mikakati ya kidijitali pia itachangia kujumuisha na kuboresha maisha ya watu wengi zaidi katika mfumo wa kifedha, iliyozidi kuongezeka nchini Tanzania na barani Afrika.

Katibu Mkuu Mtendaji wa PAPU, Sifundo Chief Moyo, alimwambia Naibu Katibu Mkuu kwamba Umoja huo unatekeleza mikakati muhimu ili kufikia maono ya waanzilishi wake ya kuiunganisha Afrika kupitia Posta.

Aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuunga mkono Umoja huo na kuwezesha kukamilika jengo la makao makuu ya PAPU jijini Arusha, Tanzania.

Jengo hilo, refu kuliko yote Kanda ya Kaskazini, limejengwa kwa ubia kati ya Umoja huo (PAPU) na Serikali ya Tanzania, kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Kamati za PAPU zinazokutana Arusha kati ya Agosti 24 na 28 zinahusika na Utawala na masuala ya kiufundi. Zitafuatiwa na mkutano wa Baraza la Utendaji la Umoja huo.

PAPU, yenye makao makuu yake Arusha, imepanga mikutano kadhaa itakayotanguliwa na uzinduzi rasmi wa jengo la Umoja hupo Septemba 2; utakaofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Mikutano hiyo ni pamoja na wa mawaziri wa sekta ya Posta Septemba 1, 2023.

Shirika la Posta Tanzania (TPC) ni miongoni mwa taasisi 21 za Afrika zinazotekeleza mikakati ya kujipanga upya kutumia TEHAMA kutoa huduma.

Chini ya Mpango wa Tanzania ya Kidijitali, TPC imefungua vituo vya huduma za pamoja na huduma mbalimbali za serikali na taasisi za umma zinapatikana. Hizo ni pamoja na usajili wa kampuni, maombi ya pasipoti na vibali mbalimbali.



# Wananchi wakabidhiwa mradi wa bil.25/- kuuendeleza

**Na Daniel Sabuni,**
SIMANJIRO

SHIRIKA la World Vision limekabidhi rasmi mikononi mwa wananchi wa Ruvuremit, Wilaya ya Simanjiro na Lembeni, Wilaya ya Mwanga, mradi wa Sh. bilioni 25.6 baada ya kuuendesha kwa miaka 25.

Mradi huo wa maendeleo wa Ruvuremit AP, unaohusisha sekta za kilimo, uchumi, afya, elimu na utamaduni, umewanufaisha kwa kipindi hicho wakazi 43,617.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Shirika la Worldvision Tanzania, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu, Subira Mwamaso, akizungumza wakati wa makabidhiano ya mradi huo mwishoni mwa wiki, alisema ukomo wake wa kuuendesha tamati yake ni Agosti mwaka huu.

Alisema mradi huo ulikuwa ukifadhiliwa na Shirika la Worldvision ya Marekani.

Kabla ya kuukabidhi mradi, Mwamaso, aliwasihi wakuu wa wilaya za Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera na Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro, Abdallah Mwaipaya, kuhakikisha jamii inaitunza miundombinu ya sekta mbalimbali iliyojengwa na mradi ili iweze kuwa endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Makabidhiano ya mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 1998, yalifanyika katika Kijiji cha Ruvuremit, Wilaya ya Simanjiro.

Baada ya makabidhiano, Mwenyekiti wa mradi huo, ambaye ni Diwani wa Kata ya Lembeni, Wilaya ya Mwanga, Iddi Seleman, alisema chanzo cha mradi huo ni matokeo ya utafiti kuonyesha matatizo katika sekta za kijamii, kama afya, elimu, kilimo, uchumi na utamaduni.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, mradi wa Ruvuremit ulitekelezwa katika Tarafa ya Ruvuremit, kwenye kata mbili za Ruvuremit na Loibosoit na Tarafa ya Lembeni katika kata tatu za Mgagao, Lembeni na Kirya.

"Vijiji 16 vya tarafa zote mbili, zimewanufaisha pia watoto 24,625, ambapo wa kiume ni 11,580 na wa kike 13,045.

...Lakini wanaume 8,475 na wanawake 10,517, ambao walikuwa wakijishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji, biashara na uvuvi," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema Mradi wa Ruvuremit kwa kushirikiana na wadau pamoja na serikali, umefanya mambo mengi ambayo yamechangia kuleta mabadiliko chanya, hasa kwenye sekta ya kilimo.

Alitaja baadhi ya mafanikio hayo ni kuwezesha kilimo chenye tija kwa kutoa mafunzo ya kilimo bora, kuboresha kilimo cha umwagiliaji na kuanzisha vikundi vya kuweka na kukopa 144. Mengine ni kujengwa kwa maghala makubwa matatu ya kuhifadhia mazao, mashine 102 za kutotoleshea vifaranga, kuku chotara 720, mbegu bora ya vifaranga wa samaki na kusaidia zaidi ya Sh. milioni 130 kama mikopo katika sekta kadhaa ikiwamo kilimo.

Katika Sekta ya Afya, alisema WorldVision ilisaidia kuwezesha wahudumu wa afya wa jamii 38, kujenga zahanati nne na nyumba za wauguzi katika Kijiji cha Loiborsoit, Ruvuremit Ngage na Gunge.

Vilevile, umewezesha upatikanaji wa viti mwendo kwa watoto wenye ulemavu 15 katika vijiji vya Mgagao, Lembeni, Mangara na Kiasangara.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera, alilishukuru Worldvision kwa upendo wake kwa wananchi wa wilaya za Simanjiro na Mwanga, kwa kuwaletea mradi kwa mika 25 uliosheheni mafanikio katika sekta nyingi na kuahidi kulinda kila kilichoachwa kwa manufaa ya wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (katikati), akiwa na mchimbaji maarufu wa madini ya Tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani, Bilionea Saniniu Laizer (kushoto) na Diwani wa Kata ya Endiamtu, Lucas Zacharia, wakijadili namna wachimbaji watakavyosaidia jamii inayowazunguka (CSR) kupitia miradi mbalimbali juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# TRA yawapa 'meno' watumishi wake ukusanyaji kodi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Tanga imewapa 'meno' maofisa wake wanaofuatulia makusanyo ya kodi mitaani na mipakani ikiwataka kutopepesa macho dhidi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu ambao wanaingiza bidhaa mbalimbali nchini kwa njia ya magendo.

Akizungumza na wafanyabiashara mwishoni mwa wiki, Meneja wa TRA, mkoani humo, Thomas Maseje, alisema katika mkoa huo, baadhi ya wafanyabiashara hivi sasa wanaathiri ukusanyaji wa mapato ya serikali kutokana na kukwepa kulipa kodi ili kupata faida kubwa na hivyo kuathiri pato la taifa

"Nitoe wito kwa viongozi wa vyama vya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuendelea kushirikiana na TRA kufichua na kukemea udanganyifu unaofanywa na baadhi ya waingizaji wa mizigo nchini ili kunusuru mapato ya serikali, afya za wananchi wetu pia kwa usalama wa nchi yetu," alisema.

"Mkoa wetu bado una tatizo kubwa la magendo ambayo husababisha upotevu mkubwa wa mapato ya serikali, mathalani kwa kipindi cha kuanzia Januari 2023, TRA imekomboa zaidi ya Sh. milioni 130 ikiwa ni kodi pamoja na adhabu kwa mizigo ya magendo iliyokamatwa," alifafanua.

Hata hivyo, alisema kuwa jabeti ya mwaka 2023/24 ni Sh. trilioni 44.36 na TRA imepewa jukumu la kukusanya Sh. trilioni 26.73 ambalo ni ongezeko la Sh. trilioni 3.08 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2022/23.

Alisema: "Kwa mkoa wetu wa Tanga, mwaka huu tumepewa lengo la kukusanya Sh. bilioni 215.04, mwaka 2022/23 lengo lilikuwa ni Sh. milioni 232.64 na tulikusanya Sh. milioni 214.39 sawa na asilimia 92,

"Mafanikio haya ni yetu sote ninyi wafanyabiashara kwani kodi mnayolipa na kukusanywa na TRA hutumika katika ujenzi wa taifa letu kwa kuboresha huduma za kijamii na kujenga miundombinu kwa ustawi wa wananchi wote," alisema.

Pia aliwaomba wafanyabiashara kutoa ushirikiano katika ukusanyaji wa kodi, akisema TRA imepanga kuendelea kutoa elimu kupitia njia mbalimbali ikiwemo ya kukutana na wadau mara kwa mara ili kuweza kutatua kero mbalimbali zinazoweza kuathiri makusanyo ya kodi.

# Waumini kanisa waandamana kupinga vitendo vya ushoga

**Na Getrude Mpezya,**
ARUMERU

WAUMINI wa Kanisa la Huduma ya Ukombozi lililopo Maji ya Chai, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, wameandamana kupinga mapenzi ya jinsia moja, huku nabii wa kanisa hilo, Rabiel Akyoo, akiwaasa wazazi kusimama katika nafasi zao za malezi kwa watoto wao ili kuepusha hasira ya Mungu.

Maandamano hayo yalilenga kupinga na kukataa matendo yote yanayohusiana na mmomonyoko wa maadili, kwa kuwa vinakwenda kinyume na mila na desturi za Mtanzania.

Akizungumzia uamuzi walioufanya jana, Nabii Akyoo, alisema walikuwa wakipeleka ujumbe kwa serikali na kuwahasa wazazi kukemea vitendo hivyo ilikuepuka kushiriki dhambi hiyo badala yake wazazi hao kusimama katika nafasi zao za malezi kwa watoto.

Nabii Rabiel Akyoo, alisema kuwa kila mzazi anapaswa kukemea hali yoyote anayoiona ni ya tofauti na kusudi la Mungu ama malezi ya wazazi likemewe kwa haraka.


"Unapoona mtu anafanya mambo mabaya lazima umkemee ili atoke pale alipo, unapomwonea haya na kumwogopa kwa sababu anakupa matumizi ama anakulisha hata wewe utakwenda jehanamu,"alisema.

Pia aliwahasa vijana kujitumaa katika kazi yoyote hata kama haujasoma wajiajiri kwa kufanya vibarua na kwa kufanya biashara hata kama ni ndogo, ni heri ukaishi maisha hata kama ni magumu lakini ukampendeza Mungu kila mmoja ajitume kwa manufaa yake na dunia nzima ili kujiepusha na tamaa," alisema.

Wema Charles, ambaye ni mzazi na muumini wa kanisa hilo, alisema kuwa uwepo wa matukio na vitendo hivyo umekuwa ukihatarisha uimara na ustawi wa familia na taifa kwa jumla.

Hata hivyo, aliwahasa wazazi kuishi katika maadili mema na malezi ambayo yatawapelekea watoto wao kuishi katika mwenendo mzuri kwenye jamii inayowazunguka.

Vilevile, Daniel Kitomari, ambaye ni mzazi aliwaomba wazazi kuacha kuwaweka watoto mbali na wao na kutengeneza upendo baina ya mzazi na mtoto ili kuweza kujua tabia na mwenendo wa mtoto na kutengeneza maadili mazuri zaidi kwa mtoto.







Vijana waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda katika eneo la Malimbe Kata ya Luchele wilayani Nyamagana mkoani Mwanza wakiwa wamebeba mizigo mikubwa na abiria juu yake ambapo ni kinyume na sheria za usalama barabarani. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Watumishi TRA waonywa kujihusisha na rushwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATUMISHI wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Kahama, wameonywa kutojihusisha katika vitendo vya upokeaji wa rushwa kutoka kwa wafanyabiashara.

Imeelezwa kuwa vitendo hivyo vimekuwa vikipunguza ufanisi kazini ikiwa ni pamoja na kukadiria mapato kidogo kutokana na zawadi wanazopewa kutoka kwa wafanyabiashara hao, hali inayosababisha serikali kukosa kodi kwa mujibu wa sheria.

Hayo yalibainishwa jana na Katibu Msaidizi Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Gerald Mwaitebele wakati wa mafunzo ya maadili kwa viongozi na watumishi wa TRA, kuwataka kufanyakazi kwa kufuata miongozo ya utumishi wa umma.

Mwaitebele alisema ili kuhakikisha wanafanyakazi ipasavyo wanatakiwa kuhakikisha wanaepuka kujihusisha na vitendo vinavyosababisha kupokea rushwa, zawadi, kukadiria kodi kubwa ambayo haipo kwa mujibu wa sheria na kwa wale watakaobainika kutenda hayo watafikishwa katika Baraza la Maadili.

"Hakikisheni mnakuwa wanyenyekevu, kujali wateja wenu, kutenda haki bila kujali dini au kabila na kufikilia kabla ya kutenda kile unachokitenda kwa mteja unayemsikiliza," alisema Mwaitebele.

Alisisitiza kuwa watumishi wanaofanyakazi kinyume na miongozo ya utumishi wa umma mwisho wake wanaishia kufukuzwa kazi na kuchukuliwa hatua stahiki. Meneja wa TRA Mkoa wa Kahama, Wariyoba Kanire, alisema mafunzo hayo yamefika muda mwafaka kutokana na uwepo wa ajira mpya kwa vijana zilizotoka hivi karibu na kuomba mafunzo hayo kuwa endelevu ili kukumbushana wajibu na kuahidi wale watakaobainika kwenda kinyume wataripotiwa.

Alisema kwa sasa hajapokea malalamiko yoyote kutoka kwa wafanyabiashara juu ya kukadiriwa kodi kubwa au watumishi wake kupokea zawadi na kutengeneza mazingira ya rushwa na hii ni kwasababu ya uwepo wa vikao vya mara kwa mara vya kukumbushana wajibu wa kufanyakazi kwa kufuata maadili ya tumishi wa umma.

Mmoja wa watumishi hao, Mayi Msoka alisema mafunzo aliyopewa yamemsaidia kutambua wajibu wake katika kazi na hivyo yupo tayari kufuata yale aliyojifunza ikiwamo kutokupokea zawadi kutoka kwa wafanyabiashara, kuacha upendeleo na kuhakikisha anatoa haki kwa kila mmoja aliyefika kupata huduma.

# M/kiti UWT akemea matukio ya ubakaji, ulawiti kwa watoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Taifa, Mary Chatanda, amekerwa na vitendo vya baadhi ya wanaume wanaofanya vitendo vya ubakaji na kulawiti kwa watoto wa kiume.

Amesema vitendo hivyo vinaathiri saikolojia ya watoto na hata kukatisha ndoto za maisha yao.

Chatanda alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Shinyanga kwenye mkutano wa hadhara baada ya kuhitimisha ziara yao ya kuzungumza na wanawake wa CCM pamona na kukagua miradi ya maendeleo katika Manispaa ya Shinyanga.

Alisema katika ziara yao hiyo moja ya agenda kuu ni kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wadogo, ambao wamekuwa wakifanyiwa na baadhi ya wanaume wasio na hofu ya Mungu kwa kuwabaka watoto wa kike na kulawiti wa kiume vitendo ambavyo ni vichafu.

"Hata kukithiri kwa magonjwa na matatizo mengi hapa duniani huenda vinasababishwa na vitendo hatari, tena unakuta mzee wa miaka 60 ana mbaka mtoto wa miaka nane si laana hii anapata, utamu gani hapo, njoo kwetu sisi watu wazima mbona ni wengi tu kwani mnakosa nini," alisema Chatanda.

Aidha, aliwataka wanawake kuungana kupinga vitendo hivyo na kuacha kuwaficha watuhumiwa, sababu vitendo hivyo mara nyingi hufanywa na watu wa karibu na familia wakiwamo wajomba, babu na hata baba mzazi wa mtoto au wa kambo.

Pia alikemea uchezaji wa vigodoro kwa kuvaa vijora vyepesi huku ndani wakiwa watupu na kisha kujimwagia maji na kuanza kucheza mbele ya wanaume.

Alisema michezo hiyo haifai kwani imekuwa ni chanzo cha wanawake kubakwa na kuwataka kucheza michezo ya asili yenye kuzingatia maadili ya Mtanzania.

Katika hatua nyingine, aliwataka wanawake kuacha kujiingiza kwenye mikopo kausha damu, ambayo imekuwa moja ya chanzo cha kufarakanisha familia zao na kuwarudisha kimaendeleo, bali wachangamkie mikopo ya halmashauri asilimia 10 isiyo na riba ambayo itaanza kutolewa hivi karibuni kwa utaratibu mzuri.

Naye Makamu Mwenyekiti wa UWT Taifa, Zainab Shomari, aliwataka wanawake katika uchanguzi zinazokuja ukiwamo uwa serikali za mitaa mwakani, wajitokeze kwa wingi kuwania nafasi za uongozi ili wapate kuingia kwenye vikao vya maamuzi.

# Mpigadebe akutwa amefariki, mwili waopolewa bwawani

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWILI wa mpigadebe katika Stendi ya Mabasi yanayofanya safari kati ya Sirari na Tarime mkoani Mara, Paschal Kirigiti umekutwa ukielea ndani ya bwawa la maji katika Mtaa wa Chomete, Kata ya Ntende.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime Rorya, Michael Njera amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema kuwa lilitoka Agosti 26, kwamba mwili wake umepelekwa katika chumba cha kuhifadhia maiti Hospitali ya Wilaya Tarime kwa uchunguzi zaidi.

"Tunaomba wananchi kutoa ushirikiano kwetu ili watuhumiwa katika tukio hilo wakamatwe," alisema Kamanda Njera.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Chomete, Kata ya Nkende, Halmashauri ya Mji Tarime, James Nyangai alisema: "Alfajili ya leo Jumamosi (juzi) wananchi waliokuwa wanakwenda kuchota maji katika bwawa lililopo hapa ambalo lipo katikati ya makazi ya watu walikuta mwili wa mtu mmoja ambaye ni kijana mwenye umri kati miaka 22 hadi 30 ukielea katika maji".

Alisema bwawa hilo lipo jirani na barabara kuu, kwamba baada ya kuuona mwili huo watu mbalimbali walijitokeza kuutambua na kubaini kuwa ni mpigadebe katika stendi ya magari madogo Sirari.

Alisema baada ya utambuzi, alitoa taarifa polisi ambao walifika na kuuchukua mwili na kuupeleka Hospitali ya Wilaya Tarime kwa uchunguzi zaidi.

Alisema: "Bwawa hili lilichimbwa na Kampuni ya COGEFA iliyokuwa ikijenga barabara mwaka 1998 na bwawa hili mbali na kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa mtaa wetu lakini limekuwa likihusika na kutokea kwa vifo vingi vya matukio ya watu kuuawa na kutupwa katika bwawa hili".

Akizungumza na waandishi wa habari, baba mzazi wa marehemu, Kirigiti Mosertega alisema: "Familia yangu tumepata pigo kwa kumpoteza kijana wetu. Tunasikitishwa kwani jana jioni alikuwa hapa Sirari hatujui alifikaje huko na kutupwa bwawani, tunaomba msaada

kutoka kwa wananchi ili wahusika katika tukio hili la mwanangu wakamatwe".

NIPASHE JUMATATU AGOSTI 28, 2023

Nipashe

Spotika



TASHA12 AKUNWA NA VIPAJI, UKURASA 14




## ISIKUPITE

Ilikuwa siku iliyojaa ushindi na dhiki kwa mshambuliaji nyota wa Arsenal Bukayo Saka baada ya winga huyo mwenye umri wa miaka 21 kuvunja rekodi ya Paul Merson ambayo ilidumu kwa miaka 26, ya kucheza mechi 82 mfululizo kwa kucheza mechi yake ya 83 mfululizo. Lakini katika hali ya ukatili wa kejeli, Saka alifanya kosa kwa kumpasia Andreas Pereira, aliyeitanguliza Fulham kupata bao wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Emirates juzi.



# TIMU SABA ZINAZOONGOZA MIKATABA MINONO YA JEZI

**LONDON,** England

KLABU za soka ziliingia mikataba ya udhamini na chapa za nguo za michezo ili kuzalisha na kusambaza vifaa vya timu na bidhaa nyinginezo. Hiki ni chanzo kikubwa cha mapato kwa klabu za soka kwani mikataba hii inazisaidia kuzalisha kiasi kikubwa kupitia chapa na uuzaji.

Dili la jezi kwa kawaida huhusisha jezi za klabu, vifaa vya mazoezi, mavazi mengine na bidhaa mbalimbali za mashabiki. Jumla ambayo chapa inalipa kwa mpango kama huo inaweza kutofautiana kulingana na umaarufu wa klabu ulimwenguni na mafanikio yake.

Ofa za vifaa si tu huchangia uimara wa kifedha wa klabu, lakini huchangia katika kuunda utambulisho wake na utambuzi wa chapa. Hii ni kwa sababu muundo au mwonekano wa seti ya timu inakuwa sehemu muhimu ya uwakilishi wake wa kuona.

Acha sasa tuangalie timu saba zilizo na ofa kubwa zaidi za jezi zinazolipwa kwa msimu...

**#7 Chelsea - Euro milioni 70 kwa msimu (Nike)**

Chelsea ilitia saini mkataba wa jezi na miamba ya nguo za michezo ya Nike ambao ulianza kutekelezwa msimu wa 2017-18. Ndio mkataba mkubwa zaidi wa kibiashara katika historia ya klabu hiyo ya Ligi Kuu England. Mkataba huo una thamani ya Euro milioni 70 kwa msimu na utaendelea kwa miaka 15 kutoka mwaka 2017.

Kabla ya kusaini mkataba huo, Chelsea ilipunguza mkataba wa Adidas uliokuwapo kwa miaka sita. Mkataba huo na kampuni ya Nike uliripotiwa kuongeza maradufu mapato ya 'The Blues' hao kutokana na makubaliano yao ya awali na Adidas.

**#6 Manchester City - Euro milioni 75 kwa msimu (Puma)**

Hili ndiyo dili pekee kati ya 10 zilizoingiza fedha nyingi zaidi duniani ambazo hazihusishi Adidas au Nike. Manchester City walitia saini mkataba huo mwaka 2019 na thamani yake ni Euro milioni 75 kwa msimu. Hata hivyo, kwa kuwa mkataba huo una miaka minne sasa na City ilishinda mataji matatu msimu uliopita, huenda ukaongezwa tena.

Mashabiki wa City wameonekana kufurahishwa na jezi ambazo Puma wameweka katika misimu ya hivi karibuni. Lakini wakati huo huo, kimekuwa kipindi kizuri cha mafanikio kwa City na mashabiki huwa hawalalamiki chochote wakati kabati ya vikombe inapokuwa imejaa.

**#5 Paris Saint-Germain - Euro milioni 80 kwa msimu (Nike)**

Umaarufu na mafanikio ya Paris Saint-Germain kwenye jukwaa la kimataifa, pamoja na kikosi chao chenye nyota wengi, uliwafanya kuwa mshirika muhimu wa Nike. PSG wameweza kusajili baadhi ya wanasoka bora duniani kama Lionel Messi, Neymar na Kylian Mbappe katika miaka ya hivi karibuni.

Umaarufu wao katika kiwango cha kimataifa umeongezeka kwa kiasi kikubwa katika muongo uliopita na imekwenda mbali sana kuwasaidia kupata mkataba wa faida wa vifaa vya Nike.

**#4 Arsenal - Euro milioni 85 kwa msimu (Adidas)**

Adidas waliongeza mkataba wao wa jezi na Arsenal Septemba mwaka jana. Kwa mujibu wa makubaliano mapya, wataendelea kutengeneza na kusambaza vifaa vya 'Washikabunduki' hao hadi 2030. Kwa mujibu wa masharti ya mkataba huo mpya, Arsenal itaingiza euro milioni 85 kwa msimu kutoka Adidas.

Adidas na Arsenal zimeripotiwa kuangazia kuwekeza katika kutengeneza safu za bidhaa kwa wachezaji na mashabiki wa kandanda na pia kuwekeza katika jamii za wenyeji.

**#3 Manchester United - Euro milioni 87.5 kwa msimu (Adidas)**

Manchester United wameweka kalamu kwenye mkataba wa jezi kubwa zaidi katika historia ya Ligi Kuu England. Mkataba huo mpya utaendelea hadi mwaka 2035 na unawakilisha nyongeza ya miaka 10 kwenye makubaliano yao ya sasa na Adidas.

Kwa mujibu wa mkataba huo mpya, Manchester United itaingiza kiasi cha Euro milioni 87.5 kwa mwaka, na kuwafanya kuwa wanaolipwa fedha nyingi zaidi kupitia udhamini wa jezi kwenye Ligi Kuu England.

**#2 Barcelona - Euro milioni 105 kwa msimu (Nike)**

Nike imekuwa msambazaji rasmi wa jezi za Barcelona tangu mwaka 1998. Pande zote mbili zimeonesha nia ya kufanya kazi pamoja na hii imesaidia uhusiano wao kukua kwa miaka mingi. Mnamo 2018, Barca iliongeza mkataba wao na Nike kwa miaka 10.

Kwa mujibu wa mkataba huo mpya, Barcelona wanapata euro milioni 105 kwa msimu kutoka kwa Nike. Ni dili la pili kwa bei ghali zaidi katika historia ya mchezo huo mzuri.

**#1 Real Madrid - Euro milioni 120 kwa msimu (Adidas)**

Kama vile Barcelona na Nike, Real Madrid na Adidas wamekuwa na ushirikiano tangu mwaka 1998. Ushirikiano huo unatazamiwa kuendelea hadi mwaka 2028 kulingana na masharti ya makubaliano yaliyokubaliwa kati ya pande hizo mbili mnamo mwaka 2019.

Real Madrid itapokea kitita cha Euro milioni 120 kwa msimu kutoka kwa Adidas na ni dili la jezi zenye faida kubwa zaidi katika historia ya soka.

# WASHAMBULIAJI 7 WENYE MABAO MENGI KARNE YA 21




**LONDON,** England

WASHAMBULIAJI wamepitia mageuzi ya ajabu katika karne ya 21.

Washambuliaji wa kisasa wamekuwa wachezaji wa aina nyingi ambao hawafungi tu kama jukumu la kitamaduni la kutafuta tu mabao. Wanatarajiwa kujumuisha matumizi mengi na kubadilika katika mchezo wa kisasa.

Washambuliaji wanatarajiwa kuchangia katika mchezo wa kujenga, kushinikiza wakiwa hawamiliki mpira na kutengeneza nafasi za mabao kwa wenzao. Mabadiliko haya ya jukumu lao yanaonesha mabadiliko ya kimbinu ambayo yametokea ndani ya mchezo.

Washambuliaji katika karne ya 21 ni zaidi ya kifurushi kamili. Ni vitisho vikali vya mabao, mahiri katika kutengeneza nafasi na kufanya kazi kwa bidii wakati hawamiliki mpira.

Hapa tunawaangalia washambuliaji saba waliofunga mabao mengi zaidi katika karne hii ya 21...

**#7 Sergio Aguero - Mabao 403**

Sergio Aguero ni gwiji wa Ligi Kuu England. Yeye ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi wa karne ya 21 na amepata mashabiki wengi duniani kote kutokana na uwezo wake wa kuzaliwa kufunga mabao.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Argentina anajulikana kwa nafasi yake na matarajio yake. Tabia hizi zimemruhusu kutumia hata uzembe mdogo wa ulinzi na kumsaidia kuwa jangili wa kweli. Lakini mchezo wa Aguero unaenda mbali zaidi ya tabia yake ya uwindaji ndani ya eneo la hatari.

Ustadi wake wa kiufundi, kasi ya haraka na umaliziaji ulimfanya kuwa ndoto mbaya kwa walinda mlango katika maisha yake yote ya soka. Aguero alifunga jumla ya mabao 403 katika mechi 730 katika karne ya 21.

**#6 Edinson Cavani - Mabao 425**

Amerika Kusini imetoa baadhi ya washambuliaji bora katika historia ya mchezo huo mzuri. Mshambuliaji wa Uruguay, Edinson Cavani bado ni mchezaji mwingine aliyeibeba Ulaya kwa dhoruba kwa umahiri wake wa kushangaza katika karne ya 21.

Cavani ni namba tisa kamili, asiyechoka uwanjani na amebarikiwa na ubunifu na ustadi wa ajabu wa kufunga. Cavani amefunga mabao 425 katika mechi 779 kwenye karne ya 21.

**#5 Zlatan Ibrahimovic - Mabao 454**

Umahiri wa kushangaza wa Zlatan Ibrahimovic ni wa kipekee kama utu wake mkubwa kuliko maisha. Aliunganisha ukubwa, nguvu na wepesi kuwazidi misuli mabeki na kutengeneza nafasi kabla ya kufunga mabao matamu.

Mabao na ushujaa wa nguli huyo wa Sweden yalionesha ubunifu wake usio na kifani na ujuzi wa kiufundi. Alifunga mabao 454 kwenye mechi 773 katika karne ya 21 ili kuimarisha sifa yake kama gwiji wa soka.

**#4 Karim Benzema - Mabao 457**

Karim Benzema ni mmoja wa wafungaji bora zaidi ambao tumeona katika karne ya 21. Udhibiti wake wa kipekee wa mpira, ustadi maridadi wa kuchezea chenga na uwezo wa kupiga pasi humfanya si mshambuliaji wa jadi tu, bali pia mchezaji mwenye nguvu. Mwendo wa Benzema ni mkali na ana ustadi.

Zaidi ya hayo, uwezo wake sahihi wa kumalizia, uchezaji wa kiungo na uwezo wa kufunga mabao unaangazia hadhi yake kama mmoja wa washambuliaji kamili wa enzi ya kisasa.

Mshambulizi huyo mashuhuri wa Ufaransa amefunga mabao 457 kwenye mechi 893 katika karne ya 21.

**#3 Robert Lewandowski - Mabao 559**

Umaliziaji usio na shaka wa Robert Lewandowski na uthabiti wa ajabu unamfanya kuwa mmoja wa washambuliaji wakubwa wa zama za kisasa.

Nyota huyo wa Poland ametumia muda wake mzuri wa kukimbia na umahiri wa angani kujitengenezea kama mashine ya kufunga mabao.

Amefunga mabao 559 kwenye mechi 773 katika karne ya 21.

**#2 Lionel Messi - Mabao 807**

Lionel Messi amechanganya usanii na usahihi kwenye medani ya soka. Udhibiti wake wa ajabu wa mpira, kupasuka kwa kasi na ustadi wa kuchezea usio na kifani umemsaidia kuimarisha ulinzi mkali katika maisha yake yote.

Messi pia ameonesha uwezo wa kufumania nyavu kutoka katika nafasi mbalimbali kuanzia pembeni hadi katikati. Amepata ustadi, upigaji wa mabao kwa mguu wake wa kushoto ni wa hatari.

Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or ni mmoja wa wafungaji bora katika historia ya mchezo huo. Amefunga mabao 807 kwenye mechi 1028 katika karne ya 21.

**#1 Cristiano Ronaldo - Mabao 819**

Cristiano Ronaldo si tu anachukuliwa kuwa mmoja wa wanasoka bora wa wakati wote, lakini kama mfungaji bora zaidi katika historia ya mchezo huo. Wasifu wa gwiji huyo wa Ureno umejaa nyakati za ustadi wa kibinafsi.


Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or ndiye mfungaji bora katika soka la kimataifa la wanaume (mabao 123). Ronaldo amefunga mabao 819 kwenye mechi 1118 katika karne ya 21.

## Nukuu


"Bado unapata nafasi nyingine mbili na usifunge - hiyo ni hadithi ya mchezo. Kiasi cha mambo tuliyofanya ili tulistahili kushinda mchezo kwa raha, sisi (hatukupaswa) kumaliza kwa pointi moja. uhakika."Tunapaswa kuonyesha kiwango kingine cha kujitolea na hamu na 'kamwe'. Ukiwa na wanaume 10, huwezi kuruhusu bao," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, akionesha kukerwa na sare ya mabao 2-2 dhidi ya Fulham waliokuwa pungufu Jumamosi.**



"Katika nyanja zote, alicheza mchezo mzuri sana katika kiwango cha juu. Alikuwa ametulia, huku hisia zikiwa zimedhibitiwa. Alikuwa na kipaji katika (kucheza) na kuleta mabadiliko. Nina furaha sana na kiwango chake," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, akipongeza kiwango cha Bruno Fernandes, baada ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Nottingham Forest juzi.**



"Nadhani yeye (Bruno Fernandes) ni mashine ya ubunifu. Kwa ujumla, nadhani Odegaard (Martin) ni mbunifu sana." Anadhibitiwa zaidi, halafu Maddison (James) pia ni mbunifu, lakini nahitaji kumuona zaidi katika timu kubwa. Kwa hiyo hilo linaweza kubadilika, lakini ndiyo maana nilimuweka namba tatu," **Kiungo fundi wa Man City, Kevin De Bruyne, akitaja viungo watatu bora katika Ligi Kuu England, wanaopenda kujitoa mhanga.**



"Katika nyanja zote, alicheza mchezo mzuri sana katika kiwango cha juu. Alikuwa ametulia, huku hisia zikiwa zimedhibitiwa. Alikuwa na kipaji katika (kucheza) na kuleta mabadiliko. Nina furaha sana na kiwango chake," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, akipongeza kiwango cha Bruno Fernandes, baada ya ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Nottingham Forest juzi.**





# TASHA12 AKUNWA NA VIPAJI, SASA KUINUA NGUMI TANZANIA

**Na Saada Akida**

NATASHA Jonas huenda likawa jina geni sana masikio mwa baadhi ya Watanzania, lakini sio jipya kwa wadau wa masumbwi (ngumi) ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Natasha ndio jina alilopewa na wazazi wake, lakini katika ulimwengu wa ndondi alibatizwa Jonas jina la babaye mzazi au Tasha12 kutokana na umahiri wake wa mchezo huo.

Jonas au Tasha12 kama anavyojiita mwenyewe ni mmoja kati ya mabondia wakubwa katika mchezo wa ngumi za kulipwa akiwa anashikilia mikanda ya ubingwa wa IBF, WBO na WBC katika uzani tofauti.

Tasha12 ambaye ni raia wa Uingereza, kwa sasa yupo nchini kwa ajili ya mapumziko yake binafsi, lakini ameamua kuchukua muda wake kwa kutembelea baadhi ya gym za mabondia wa Tanzania na ameshangzwa na mazingira aliyoyaona ya mazoezi huku wakiwa bado wanafurahia wanachokifanya.

Bondia huyo ambaye amepewa ubalozi wa Utalii, Zanzibar, amefanya mahojiano maalum Nipashe juu ya ujio wake nchini pamoja na mipango yake ya kuhakikisha mchezo wa ngumi za kulipwa Bongo unachukua nafasi kubwa.

Bondia huyo amefichua ni mara yake ya kwanza kufika Tanzania safari yake ikianzia visiwani Zanzibar alifanikiwa kupewa zawadi ya ubalozi wa utalii wa kuhakikisha anavitangaza visiwa hivyo kupitia majukwaa mbalimbali atakayokuwa akiyatumia kupigana.

"Ni mara yangu ya kwanza kuwa hapa Tanzania, lakini nilianzia Zanzibar, wamenipa ubalozi wa utalii chini ya waziri wa utalii, kwangu imekuwa faraja kubwa kwa heshima ambayo nimepewa," anasema Bondia huyo.

**Mipango yake ya kutangaza utalii wa Zanzibar**

Natasha anasema kufanya mambo mengi ya kuhakikisha Zanzibar inapokea watalii wengi ambao watakuja kutalii kwa sababu ni sehemu nzuri yenye mambo mengi ya kuvutia.

"Binafsi nimeweza kujifunza mambo mengi, uzoefu ambao nimeweza kuupata kupitia safari kubwa kuanzia visiwani hadi hapa Bara kwa sababu nilipata nafasi ya kuangalia hadi mechi ya watani wa jadi ambayo Simba walifanikiwa kushinda, ulikuwa ni mchezo wa Ngao ya Jamii," anasema Bondia huyo.

**Sapoti yake kurejea masumbwi Zanzibar baada ya miaka 60**

"Nadhani kunakuwa na programu maalum za kuendeleza na kukuza vipaji kwa lengo la kuwaendeleza na kuifanya Zanzibar ijulikane kupitia mchezo huu wa ngumi," anasema Bondia huyo wa Uingereza.

Anasema anaimani kubwa ya Zanzibar kufanikiwa malengo hayo ya kuurudisha mchezo huo kwa sababu ametembelea baadhi ya gym na kuona vipaji vingi ikiwamo mchezo huo.

**Gym za mabondia Dar es Salaam**

"Nimeona mambo mengi yamenishangaza hasa upande wa mazingira ambayo mabondia wanafanya mazoezi, lakini bado wanakuwa na furaha.

Hili jambo limenihamasisha kwa kiasi kikubwa na kuona watu wanavyojituma katika mambo wanayopenda kufanya, nitawasapoti kadiri ambavyo inawezakana ili kuifanya Tanzania kuwa mmoja kati ya taifa kubwa la ngumi," anasema Natasha.

Anasema baada ya kutembelea gym mbalimbali ameona changamoto za mabondia na anatarajia atakaporejea Uingereza atakutana na wasimamizi wake kwa ajili ya kuona jinsi gani wanaweza kunyanyua mchezo wa ngumi.

Tasha12 anasema anatamani zaidi kuona mchezo wa ngumi Tanzania unakuwa juu baada ya kuona baadhi ya mabondia kuwa na vipaji vikubwa akiwamo Hassan Mwakinyo ambaye aliweza kumshawishi kuja kufanya mapumziko yake nchini hapa.

"Mwakinyo alipokuwa Uingereza aliniambia nije kufanya mapumziko yangu hapa Tanzania, pia kupitia baadhi ya gym za mabondia na kuona vipaji, kweli vipo na ninatakapokuwa nyumbani nitakuwa balozi mkubwa wa Tanzania katika kuufanya mchezo wa ngumu unakuwa zaidi," anasema Natasha.

**JE, WAJUA?**



HAWA ndio wachezaji watano wanaopewa nafasi ya juu kutwaa Kiatu cha Dhahabu Ulaya msimu huu; #5 Goncalo Ramos (Paris Saint-Germain), #4 Robert Lewandowski (Barcelona), #3 Victor Osimhen (Napoli), #2 Harry Kane (Bayern Munich) na #1 Erling Haaland (Manchester City).





# CCM yawatoa hofu wafanyabiashara Soko la Sabasaba jijini Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, kimewatoa hofu wafanyabiashara wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma kuwa hawataondolewa mwaka huu kama walivyotakiwa na Jiji ili kupisha ujenzi wa soko la kisasa.

Mwenyekiti wa CCM mkoani hapa, Adam Kimbisa, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao kwenye mkutano wa kujadili na kutatua kero mbalimbali ikiwamo ya kuwaondoa kwenye eneo hilo.

Alisema ujenzi huo hautafanyika kwa mwaka wa fedha 2023/24 kutokana na halmashauri hiyo kutokuwa na fedha za kutosha, hivyo inategemewa katika bajeti ya mwaka 2024/25 utakapopangwa tena.

"Hivi sasa haitafanyika bomoa bomoa hadi serikali na Halmashauri ya Jiji itakapokuwa na bajeti ya fedha ya kujengea, hivyo wafanyabiashara fanyeni biashara zenu kwa uhuru mpaka pale watakapoambiwa," alisema.

Alibainisha kuwa Jiji hilo lina mpango wa kukarabati na kujenga soko hilo ili kuwa katika mpangilio mzuri wa kisasa na kuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara wengi zaidi. Kadhalika, aliagiza halmashauri hiyo kuboresha masoko yote ili kuwa na miundombinu rafiki.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema serikali itahakikisha inashirikiana na wafanyabiashara kutatua kero zao ili kuendelea kujikwamua kiuchumi.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya tume hiyo na mwelekeo wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24 jijini Dodoma jana, kwenye ukumbi wa Idara ya Habari **(MAELEZO). PICHA: PAUL MABEJA**

# Wakazi 150,000 kufanyiwa uchunguzi wa macho

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAKAZI 150,000 wa mikoa ya Singida, Morogoro na Dodoma wanatarajiwa kunufaika na huduma za uchunguzi wa macho kupitia mradi wa 'Macho Yangu' unaotekelezwa na Shirika la Sightsavers.

Mkurugenzi Mkuu wa shirika hilo, Godwin Kabalika, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mjini hapa kwenye kikao cha kutambulisha mradi huo mpya baada ya Mradi wa Boresha Macho ulioanza kufanya kazi mwaka 2019 na kufikia tamati mwaka 2022 kwenye mikoa ya Singida na Morogoro. Alisema mradi huo mpya watu 15,000, watafanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho na kutoa miwani kwa watu 15,000.

"Tutasaidia vifaa tiba vinavyohusika na macho kwenye vituo vya kutolea huduma katika mikoa ambayo mradi utatekelezwa. Mkoa wa Dodoma haukuwapo kwenye ule mradi wa awali lakini mradi huu tumeuweka kwasababu tumebaini wananchi wengi wanakabiliwa na matatizo ya macho," alisema.

Naye mratibu wa mradi huo mkoani Singida, Upendo Minja, alisema kwenye mkoa huo wananchi 50,000 watafanyiwa uchunguzi wa huduma za macho, 5,000 watafanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho na wengine 5,000 watapewa miwani katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa mradi huo.

Mratibu wa huduma za macho mkoani humo, Upendo Mwakabalile, alisema kupitia mradi wa Boresha Macho walilenga watu 5,625 kufanyiwa upasuaji wa jicho la mtoto lakini hadi mwisho wa mradi wamefanyiwa watu 7,995.

Alisema katika huduma ya uchunguzi wa matatizo ya macho, mradi huo ulijiwekea lengo la kuchunguza watu 62,500 lakini wamefanyiwa uchunguzi watu 110,834 na wengine 3,770 wamepewa huduma ya miwani kati ya lengo lililowekwa la watu 2,500 kutoa huduma hiyo.

Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji, Stanslaus Choaji, aliwaagiza waganga wakuu wa wilaya na waratibu wa macho kutoa ushirikiano kwa shirika hilo ili kuwafikia wananchi.

# Serikali yaweka mikakati kuokoa misitu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imesema imejipanga kuokoa misitu kwa kuhakikisha kunakuwapo na usimamizi shirikishi wa maliasili za misitu nchini ili kunufaisha vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), Dk. Revocatus Mushumbusi, alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipomwakilisha Kamishna wa Uhifadhi wa Misitu nchini, Pof. Dos Santos Silayo, kwenye ufunguzi wa kikao cha awali cha wataalamu wa mradi wa usimamizi shirikishi wa misitu ya miombo ya nyanda kame.

Alisema usimamizi shirikishaji wa misitu unasaidia kupunguza athari za kuteketea kwa rasilimali hiyo ambayo imekuwa ikiendelea kuteketezwa kwa kasi nchini.

Alibainisha kuwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) iliyo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) wameanza kutekeleza mradi wa uhifadhi wa misitu ya miti ya miombo nchini kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira ya Dunia wa Global Environmental Facility (GEF 7).

Alibainisha kuwa lengo kuu la mradi ni kukomesha na kubadili mwelekeo mbaya wa uharibifu wa ardhi na upotevu wa bioanuwai katika maeneo yaliyoharibiwa ya ukanda wa misitu ya miombo Kusini-Magharibi mwa Tanzania kwa kutumia mbinu shirikishi za usimamizi wa mandhari.

Kadhalika alisema mradi huo unatekelezwa katika nchi 11 ambazo ni Angola, Botswana, Malawi, Msumbiji, Namibia, Zimbabwe, Tanzania, Kenya, Burkina Faso, Mongolia, Kazakhstan. Alisema kila nchi itapimwa kwa matarajio waliyojiwekea ambapo Tanzania itapimwa kwa uhifadhi mzuri wa misitu ya miombo na hatimaye kuleta tija kwenye mnyororo mzima wa mazao ya nyuki na maisha ya jamii.

Aliongeza kuwa mradi huo unatekelezwa ukanda wa Mkoa wa Tabora (Kaliua) na Mkoa wa Katavi (Mlele) kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 6.87 sawa na Sh. bilioni 16.8 kuanzia mwaka 2022 hadi 2027.

Mratibu wa mradi huo, Zainabu Bungwa alisema Tanzania ni ya pili kwa ukubwa kidunia kuhusu mtawanyiko wa misitu ya miombo ambapo ni asilimia 90 ya misitu yote iliyopo hapa nchini.

Alisema ekari 469,000 za misitu zimekuwa zikiharibiwa kwa mwaka hapa nchini, hivyo jitihada zinahitajika kulindwa kwa mazingira hayo.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Martha Kalowela, alisema mchakato wa mradi huo ulianza mwaka 2018 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa sekta ya misitu.

# TANROADS: Ujenzi barabara ya mzunguko kukamilika Desemba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta, amesema ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje eneo la Nala -Veyula na Ihumwa Bandari Kavu unatarajia kukamilika Desemba mwakani.

Mhandisi Besta aliyasema hayo jana kwenye ziara ya kutembelea maendeleo ya ujenzi wa mradi huo jijini hapa.

"Tunatarajia ujenzi huu utakamilika kama ilivyopangwa nawaomba wananchi msiwe na wasiwasi wowote juu ya suala la ujenzi wa mradi huu," alisema.

Akizungumzia kuhusiana na vifaa vya ujenzi huo, alisema wamekuwa wakipima katika maabara mbalimbali ikiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na maabara nyingine ili kuhakikisha wanatumia vifaa bora vyenye viwango ambavyo vitaifanya barabara hiyo idumu kwa muda mrefu.

"Tunahakikisha viwango vyote vya ubora vinazingatiwa, lengo ni kutaka barabara yenye viwango vya juu, vinavyohitajika," alisema.

Alisema mkandarasi anapoleta vifaa katika mradi huo anapaswa kutoa taarifa na sampuli zinachukukiwa kupelekwa maabara kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi.





## TARURA yapewa maagizo ujenzi barabara Ndulilo-Itete

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MKUU wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, amezindua ujenzi wa Barabara ya Ndulilo - Itete inayounganisha Kata ya Lufingo na Kyimo ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami, huku akiagiza isimamiwe vizuri ili ijengwe kwa kiwango kinachotakiwa.

Barabara hiyo ni miongoni mwa barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na ina urefu wa kilomita 11.38 ambapo inajengwa kwa Sh. bilioni 8.9.

Alisema mradi huo ukikamilika utawarahisishia wananchi shughuli za usafiri na usafirishaji hasa wa mazao ya biashara ambayo wanazalisha katika maeneo hayo ambayo ni ndizi, chai na maparachichi.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya hiyo ikilenga kuwaondolea wananchi kero ambazo walikuwa wanazipata kwa muda mrefu hasa katika sekta za usafirishaji, elimu, afya, maji na umeme.

"Leo tunashuhudia uzinduzi wa barabara hizi lakini vituo vya afya, vyumba vya madarasa pamoja na miradi ya maji inasambazwa kwa kasi huko vijijini, barabara hii ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao kwenda sokoni," alisema Haniu.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa mkandarasi anayetekeleza mradi huo na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kurudisha nyuma maendeleo ya mradi ikiwamo vitendo vya uwizi wa vifaa vya ujenzi.

Katika hatua nyingine, Haniu aliwataka wananchi wanaopitiwa na barabara hiyo kutokwamisha mradi kwa kudai fidia kwa maelezo kuwa barabara hiyo ni kwa ajili ya faida yao wenyewe na kwa eneo kubwa inapita kwenye ile ya zamani.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Rungwe, Mekson Mwakipunga, aliishukuru serikali kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi ya chama hicho kwa vitendo hasa kwenye uboreshaji wa miundombinu.

Alimtaka mkandarasi anayejenga barabara hiyo kutoa ajira kwa wazawa wa maeneo hayo kwa maelezo kuwa utaratibu huo utaongeza mzunguko wa fedha kwenye eneo hilo na kuwafanya wananchi kuwa sehemu ya mradi.

# Maofisa ugani wapigwa msasa matumizi vifaa vya kisasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Kilimo imeanza kutoa mafunzo maalumu kwa maofisa ugani wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu matumizi sahihi ya zana na vifaa vya kisasa vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa mwishoni mwa wiki kwa maofisa hao kutoka katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Njombe, Katavi na Songwe ambapo wanapatiwa elimu kuhusu matumizi ya vifaa vya kidigitali vya kupimia afya ya udongo.

Vifaa hivyo vimenunuliwa na serikali na kusambazwa kwa maofisa ugani kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kubaini afya ya udongo kwenye mashamba yao hasa kukabiliana na tindikali ambayo imekuwa ikiathiri uzalishaji.

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Mhandisi Juma Mdeke, alisema serikali imenunua vifaa hivyo kwa lengo la kuwasaidia wakulima na siyo shughuli zingine.

Alisema mbali na vifaa hivyo pia serikali imenunua pikipiki na kuwagawia maofisa ugani hao kwa lengo la kuwarahisishia kazi ya kuwafikia wakulima katika maeneo yao.

Alisema ili kudhibiti vifaa hivyo visitumike kwa shughuli tofauti na za kilimo, vifaa hivyo vimefungwa mifumo maalumu ya ufuatiliaji ambayo huwadhibiti maofisa hao wasitoke navyo nje ya maeneo yao ya kazi.

"Tulibaini kwamba kuna baadhi ya maofisa hawa wanaweza wakawa wanavitumia vifaa hivi tofauti na malengo, kwa hiyo tuliamua kuviwekea mfumo maalumu ambao unatusaidia kuona kila anachofanya ofisa kilimo," alisema Mdeke.

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Viwanda na Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Anna Mwambene, aliwataka maofisa ugani kuepuka kutumia vifaa hivyo kwa maelezo kuwa wakifanya hivyo watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema serikali iliamua kuweka mfumo wa kudhibiti matumizi ya vifaa hivyo baada ya kubaini baadhi ya maofisa hao walikuwa wanatumia kwa shughuli tofauti.

Alisema baadhi ya maofisa hao walikuwa wanatumia pikipiki walizopewa na serikali kufanyia biashara ya kubeba abiria na baadhi yao walikuwa wanakwenda nazo mpaka nje ya nchi hali ambayo ilikuwa inasababisha vifaa hivyo kuharibika na vingine kupotea.

"Jukumu lenu maofisa ugani ni kuwafundisha wakulima mbinu bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji, sasa serikali imewawezesha hivi vifaa ili kuwaongezea ufanisi, hakikisheni mnavitumia kwa shughuli iliyolengwa," alisema Mwambene.

Baadhi ya maofisa ugani walioshiriki mafunzo hayo walishukuru serikali kwa mafunzo na vifaa hivyo wakieleza kuwa watavitumia kwa ufanisi ili kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji.

Mmoja wa maofisa hao, Enock Ndunguru alisema mafunzo hayo yatawawezesha kuelewa vizuri miiko na taratibu za kutumia vifaa hivyo na hivyo kuepuka kuingia katika migogoro na serikali.

Alisema kutokana na kutopatiwa mafunzo baadhi ya maofisa hao walikuwa wanazitumia pikipiki hizo kwenye shughuli ambazo hazihusiani na kilimo huku baadhi wakizitumia mpaka usiku.



Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, akizungumza na mmoja wa wazazi waliowapeleka watoto wao kwenye uchunguzi na matibabu ya macho katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya alipotembelea kambi maalum inayowashirikisha madaktari bingwa kutoka Ujerumani. **PICHA: NEBART MSIKWA**

# RUWASA: Marufuku kufanya shughuli kwenye vyanzo vya maji

**Na Elizabeth John,** WANGINGLOMBE

WANANCHI wilayani Wanging'ombe katika Mkoa wa Njombe, wametakiwa kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji ili wasiviharibu na kusababisha uhaba wa maji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), Mhandisi Ruth Koya alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki baada ya kutembelea mradi wa maji wa Igando-Kijombe wilayani humo.

Mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya STC JV YELL LTD kwa zaidi ya shilingi bilioni 12 ambapo unatarajiwa kuwahudumia zaidi ya wananchi 14,377 wa vijiji 10.

"Tunawaomba wananchi waendelee kushirikiana na sisi hasa katika utunzaji wa vyanzo vya maji kama tulivyopata taarifa kwamba chanzo cha maji ni mto, mazingira ya mto yanatakiwa yatunze maji maeneo yale wananchi wasifanye shughuli za kibinadamu," alisema Mhandisi Koya na kuongeza.

"Maeneo hayo wakifanya shughuli za kibinadamu wataathiri kile chanzo, wataathiri ubora wa maji kwa hiyo watakaoathirika zaidi ni wao wenyewe, kwa hiyo tunawaomba sana watunze vyanzo vya maji ili waendelee kupata huduma na miradi yetu ya maji iwe endelevu," aliongeza. Alisema kuwa asilimia 80 ya Watanzania wapo vijijini na kwamba nia ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani.

"Sisi ndiyo tunapeleka maji vijijini RUWASA na tunatakiwa kufanye kazi kwa bidii kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi wapo vijijini na tumepewa jukumu la kuwahudumia wananchi," alisema Mhandisi Koya.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Malangali, Esau Sanga, alisema kuwa mradi huo utasaidia wananchi kuondokana na adha ya upatikanaji wa maji sambamba na kuhakikisha wanaelimisha wananchi kuacha kujishughulisha na shughuli zozote kwenye vyanzo vya maji.

"Mimi niwahakikishie kwamba hatutakubali sisi kutokana na hili wananchi waendelee kufanya shughuli kule, tutawakataza na tutawapa elimu na tulishaanza kuwapa elimu kwa hiyo kazi ikikamilika hatua mtu yeyote atakayeendelea kufanya shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo," alisema Sanga.

Awali Mkurugenzi wa Ufundi kutoka RUWASA, Ndele Mengo, alisema mradi huo ni moja kati ya ile miradi korofi 177 iliyopo nchini. "Huu mradi tuliurithi ukiwa bado haujakamilika lakini mpaka sasa hivi umeshakamilika, vijiji viwili vimeshaanza kupata huduma ya maji lakini lengo letu ni kupeleka katika vijiji vyengine ambavyo tunaendelea navyo kwenye bajeti nyingine," alisema Mengo.

Meneja wa RUWASA, Mhandisi Sadick Chaka, alisema wanakabiliwa na changamoto ya kupungua kwa maji katika vyanzo kutokana matumizi ardhi yasiyofaa.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Wanging'ombe, Mhandisi Josh Chum alisema mradi huo ulianza mwaka 2018 na hivi sasa umefikia asilimia 92.3 na umeanza kutoa huduma katika Kijiji cha Malangali.

Msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Emmanuel Ndosi kutoka Kampuni ya STC JV YELL LTD alisema watahakikisha kwa muda uliobaki wanakamilisha kazi zote ili wananchi waweze kupata majisafi na salama kwa wakati.



## Rais Samia: Tuongeze vivutio vya utalii, tuvutie wageni

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan amesema kuna haja kwa Zanzibar kuongeza vivutio vingi vya utalii kwa kubuni matukio maalumu ya kuwavutia wageni na kuviimarisha vivutio vya asili.

Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa Tamasha la Kizimkazi katika Uwanja wa Paje Mkoa wa Kusini Unguja, hotuba yake ikisomwa na Rais za Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema tamasha hilo linatoa fursa ya kuendeleza utalii na kuutangaza Mkoa wa Kusini kiutalii na Zanzibar kwa kufungua fursa nyingi za maendeleo ikiwemo biashara, uwekezaji na uchumi.

Alisema matarajio yake ya baadae kwa tamasha hilo kuweka historia nyingine ya Mkoa wa Kusini Unguja kwa kuongeza fursa nyingi za utalii, uwekezaji na maendeleo ya biashara.

Aidha, alisema tamasha hilo mbali na kuongeza vivutio vya utalii vya ndani ya mkoa huo kama tukio la asili la 'mwaka kogwa' lakini kuendelea kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa kuendeleza umoja na mshikamano wa Watanzania.

Katika hotuba hiyo, Dk. Mwinyi alisema tamasha hilo limeendelea kuenzi na kuimarisha utamaduni wa Tanzania kwa kuvienzi vyakula vya asili, kuimarisha makongamano, michezo, burudani na kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kubuni miradi ya maendeleo kwa kukuza biashara.

Hata hivyo, Rais Dk. Mwinyi alipongeza Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja na kamati ya maandalizi ya Tamasha la Kizimkazi kwa kuelendeza juhudi za Rais Dk. Samia kwa kulienzi tamasha hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja Rashid Hadidi aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wanatoa kukuza maendelo ya mkoa huo.

# Mwinyi azindua ujenzi wa kituo cha afya chenye hadhi maalum

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amezindua ujenzi wa Kituo cha Afya Kizimkazi kilichoko Mkoa wa Kusini Unguja, kinachojengwa na serikali kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) ikiwa ni jitihada za wadau hao wawili kuimarisha huduma za afya kwa wananchi.

Hafla ya uzinduzi huo ilifanyika jana, ikihusisha uwekaji wa jiwe la msingi eneo unakotekelezwa mradi huo, ikiwa pia ni sehemu ya uzinduzi wa Tamasha la Kizimkazi 2023.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi waandamizi kutoka serikalini akiwamo Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidh, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi, viongozi waandamizi wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, pamoja na wakazi wa eneo hilo.

Akizungumzia mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 4.4 (NBC imechangia Sh. milioni 400), Rais Mwinyi pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa hatua hiyo, alisema ni adhma ya serikali kuboresha huduma ya afya kwa kujenga vituo vya afya vyenye hadhi ya kipekee katika baadhi ya maeneo kulingana na uhitaji mkubwa wa huduma hiyo katika maeneo hayo.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni pamoja na eneo la Tumbatu, Fuoni na Kizimkazi, akifafanua "...kimsingi kwa sasa ujenzi wa miundombinu kwenye sekta ya afya ndio kipaumbele chetu.

"Jitihada ambazo zitafuatiwa kwa ukaribu sana ni upatikanaji wa wataalamu wa afya pamoja na vifaa tiba. Kituo hiki cha Kizimkazi ni moja ya vituo vitatu vya afya vinavyojengwa katika mpango wa ujenzi wa vituo vyenye hadhi maalum hapa Zanzibar.

"Kipekee sana niwashukuru wadau wa maendeleo ikiwamo Benki ya NBC kwa kutuunga mkono kwenye hili na ni matumani yangu kwamba msimu ujao wa Kizimkazi Festival tutazindua kituo hiki kikiwa kimekamilika."

Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidh, alisema kukamilika kwa kituo hicho kutawezesha utoaji huduma kwa wagonjwa takribani 8,000 kwa wakati mmoja huku akibainisha kuwa kituo hicho kitahusisha huduma za kliniki, kujifungua, vipimo vya maabara, huduma za meno, uchunguzi wa X-ray na ultrasound.

"Pamoja na kuboresha afya ya jamii kwa ujumla, kituo hiki kitawasaidia sana hasa kinamama hususani wakati wa kujifungua, wagonjwa wa nje na wagonjwa wanaohitaji huduma ya kulazwa," alisema.

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema mradi huo ni sehemu ya mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo kushirikiana na serikali katika kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii ikiwamo changamoto ya afya.

"Tunaamini kwamba kuwa kituo hiki kitatoa huduma bora za afya kwa wanawake na watoto wa Kizimkazi na maeneo jirani.

"Kupitia ushirikiano wetu na Taasisi ya AMREF, pia tumefanikiwa kuimarisha afya ya uzazi kwa kinamama. Tumesaidia kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali mbalimbali visiwani Zanzibar hasa kwa ajili ya matibabu wakati wa kujifungua," alisema.

Kwa mujibu wa Sabi, mbali na ujenzi wa kituo hicho cha afya, benki hiyo pia imekuwa ikishiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa madarasa ya chekechea, ununuzi samani za ofisi kwenye Saccos ya wakazi wa eneo hilo na mwaka 2021 benki hiyo ilianzisha mradi wa Mobile Clinic (Kliniki Inayotembea) ambapo kupitia kwake imeweza kutoa huduma za afya kwa wajawazito zaidi ya 4,000.

Jitihada za benki hiyo kwenye sekta ya afya zinakuja siku chache tu baada ya kufanyika kwa mbio za NBC Dodoma Marathon, ambapo hadi sasa zimefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. milioni 500 kwa ajili ya kutoa elimu na kupambana na saratani ya shingo ya kizazi inayoongoza kwa vifo kwa wanawake sambamba na kufadhili masomo ya wakunga ili kuokoa maisha ya kinamama na watoto wakati wa kujifungua.

Mbali na uzinduzi huo, Rais Mwinyi pia alipata wasaa wa kutembelea banda la maonesho la benki hiyo lililoko viwanja vya Paje, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja, ambako uzinduzi wa Tamasha la Kizimkazi ulifanyika.



Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy, alipotembelea mabanda ya maonesho siku ya ufunguzi rasmi wa tamasha la Kizimkazi linaloendelea katika Viwanja vya Kashangae vilivyopo Paje, visiwani Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kampeni ya kupunguza vifo vya mama, mtoto yazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Kimataifa la AMREF kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar, imezindua kampeni ya uzazi ni maisha ili kusaidia upatikanaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Akizindua kampeni hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Maisara Mjini Unguja, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi alisema uzinduzi wa kampeni hiyo ni kuthamini umuhimu wa haki ya maisha hasa kwa kuboresha afya ya mama na mtoto.

Alisema kiwango cha vifo vinavyotoka na uzazi kwa kinamama na watoto Zanzibar bado lipo juu na kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa kinamama 134 hufariki kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka na vifo 28 vya watoto wachanga kati ya vizazi hai 1,000.

Dk. Mwinyi alisema kiwango hicho kinasababishwa na changamoto mbalimbali zinazohusiana na huduma za mama na mtoto katika hospitali na vituo vya afya ikiwamo upungufu wa vifaa tiba, uhaba wa wahudumu na kukosekana kwa dawa.

"Ni matumaini yangu kupitia kampeni hii tutapiga hatua katika kukabiliana na hali hii ambapo itawezesha kupatikana vifaa tiba kwa vituo vya afya 28 sawa na asilimia 40.5 ya vituo vyote 69 vinavyotoa huduma za mama na mtoto Zanzibar"alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema hatua hiyo sambamba na jitihada za serikali za kuimarisha huduma za afya ya msingi hasa kwa ajili ya uzazi, italeta mafanikio makubwa katika kulinda maisha ya mama na mtoto.

Naye Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema lengo la kuanzishwa kwa kampeni hiyo ni kupunguza vifo vya wajawazito na watoto nchini.

Alisema katika kulikabili tatizo hilo kivitendo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mikakati madhubuti ikiwemo kuwachukulia hatua kali za kisheria na nidhamu watumishi wote wa sekta ya afya wanaokiuka sheria na taratibu za utumishi wao.

Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la AMREF Afrika kwa upande wa Tanzania, Dk. Folence Temu alisema lengo la kuanzishwa kampeni hiyo ni kukusanya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununuliwa vifaa tiba vya hospitali na vituo vya afya 69 vinavyotoa huduma za mama na mtoto, Zanzibar.

Alisema wakiwa kwenye mwaka wa pili wa kampeni yao, wamefanikiwa kukusanya Sh.milioni 557 na wamepokea ahadi za shilingi milioni 883 ambayo itafikisha lengo la kampeni hiyo kufikia 2024.

Katika uzinduzi huo, AMREF iliikabidhi Wizara ya Afya gari linalotoa huduma za afya likiwa linatembea, ambalo litasadia katika uharakishaji wa utoaji wa huduma za afya kwa mama na mtoto.

# Kamati ya Bunge yapongeza mazingira bora ya uwekezaji

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeipongeza serikali kwa kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini, ikiwamo kuhakikisha kunakuwa na mifumo madhubuti ya usalama na afya mahali pa kazi.

Pongezi hizo zimetolewa jana na kamati hiyo ilipofanya ziara katika viwanda vya mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa lengo la kufuatilia uzingatiaji wa taratibu muhimu za usalama na afya kazini miongoni mwa waajiri nchini.

Katika viwanda vya Bakhresa Flour Mill kilichoko Buguruni, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Hassan Toufiq, aliipongeza serikali kwa kuwawezesha wawekezaji nchini kuwa na uzalishaji endelevu na wenye tija.

"Ziara hii ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yetu ya kawaida na tumefurahi kuona wenye viwanda tuliowatembelea leo wamepata mafanikio makubwa katika shughuli zao kwa kuwa wanafanya uzalishaji mkubwa wa bidhaa zinazouzwa ndani na nje ya nchi yetu. Wawekezaji hawa wamekiri kupata ushirikiano mkubwa kutoka serikalini ikiwamo Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), ambao wamekuwa wakiwasaidia katika kuweka mifumo ya kudhibiti ajali na magonjwa pamoja na kufanya ukaguzi wa mifumo ya umeme na mitambo ya uzalishaji jambo ambalo limesaidia kuongezeka kwa ufanisi wa mitambo husika pamoja na kuiweka katika hali ya usalama wakati wote," alisema Toufiq.

"Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hasa kwa wawekezaji wa ndani. Tunaishauri serikali kuendelea kujenga mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji ili wawekezaji wetu wazidi kukua na kuongeza mtandao wa uzalishaji wao ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu," alisema Toufiq.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Boniface Mwita, alisema uwekezaji nchini kwa kiwango kikubwa bado unategemea nguvukazi zaidi hivyo ni muhimu kuwekeza katika mifumo ya kulinda afya na usalama wa wafanyakazi.

Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Jamal Katundu alisema: "Kwa kuzingatia wajibu wa Wizara ya Kazi na Taasisi chini yake ambao ni kusimamia uwepo wa mazingira mazuri ya kazi na kuhakikisha kwamba viwango vya kazi vinazingatiwa, tutaendelea kutekeleza wajibu huo ipasavyo kama tulivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais Samia tangu alipoingia madarakani.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, aliwashukuru wawekezaji kwa kutambua mchango wa OSHA katika kukuza biashara zao na kuahidi kuendelea kushirikiana nao katika kuboresha mifumo ya usalama na afya mahali pa kazi.



Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Rehema Sombi (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi kitabu cha 'The First Female President' kilichoandikwa na mwanafunzi wa darasa la sita, Rafat Simba (wa pili kushoto), dhima ya kitabu hicho ni kuhamasisha watoto kusimamia ndoto zao bila kukata tamaa, uzinduzi huo ulifanyika jana mkoani Dar es Salaam. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Maofisa ugani sasa kutoa taarifa za kazi kila siku

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Kilimo wako kwenye hatua za mwisho za maandalizi ya kuanzisha mfumo maalum utakaowezesha maafisa ugani kutoa taarifa zao za kazi za kila siku ili kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo hasa baada ya maboresho makubwa yanayoendelea kufanywa sambamba na ugawaji wa vitendea kazi vya kisasa kwa wataalamu wa sekta hiyo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema hayo mjini Morogoro alipokutana na maofisa ugani 132 kutoka mikoa ya kanda za Mashariki na Kusini waliokuwa wakielimishwa kuhusu usimamizi na matumizi ya vitendea kazi vya kisasa vya kilimo vilivyotolewa na serikali.

Alisema pamoja na kupewa vifaa kazi mbalimbali ikiwamo vishikwambi, pikipiki, vifaa vya kupimia afya ya udongo na vifaa vingine, kwa sasa Wizara ya Kilimo imeagiza magari kwa kila mkoa ili kuwawezesha maofisa ugani kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Pia wizara hiyo iko mbioni kuanza kuwajengea nyumba maofisa ugani ili waweze kuishi jirani na maeneo yao ya kazi na kuwahimiza kuwa vifaa wanavyopewa vinaleta tija kwa maendeleo ya sekta ya kilimo.

"Heshimisheni wizara kwa kufanya kazi kwa bidii, mna vishikwambi, vinapiga picha, vinachukua alama za vidole, vinachukua namba muhimu za mashamba, ikizingatiwa umiliki wa mashamba unabadilika mara kwa mara, leo huyu kalima ekari mbili, kesho ameuza moja amebaki na moja, sajilini wakulima na mkifanya kazi yenu vyema mtajenga vyema heshima yenu wenyewe," alisema.

Alisema mikakati ya wizara hiyo ni kurasimisha biashara ya kilimo nchini ikiwamo kwa kuanzisha vituo vya kuuza mazao baada ya kubaini halmashauri nyingi za wilaya zinapoteza fedha nyingi kwa kukosekana kwake, kusajili na hata kusimamia suala zima la utoaji wa vibali vya kuuza mazao kutoka wilaya moja kwenda nyingine.

"Kwa sasa wizara imeweka mkazo kwenye vipaumbele vitatu vikubwa, na kubwa na kuu ni tija, tumekusudia kuongeza tija kwenye kilimo, mbegu bora zipatikane, na zipatikane kwa wakati, wakulima waelimishwe kuhusu mbegu bora zinazoendana na udongo wa hali ya maeneo yao, lakini pia tunaangalia uimarishaji wa huduma za ugani kwa kuziimarisha na kuongeza maeneo ya umwagiliaji," alisema Mweli.

Alimpongeza Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya mji wa Kibaha mkoani Pwani, Joseph Njau kwa utendaji kazi bora na wenye tija kwa wakulima na kutaka wengine waige mfano wake.

"Ninataka mfahamu kuwa kila serikali inayo namna yake ya kuona uwezo na moyo wa utendaji kazi wa mfanyakazi wake hivyo kila mnapofanya kazi kwa bidii mtaonekana tu, huyu bwana nilikuwa simjui na sina hata namba yake ya simu, lakini Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nikson Simon alinipigia simu na kunielezea sifa zake."

Alipohojiwa Njau siri ya sifa hizo, alisema amekuwa na ushirikiano na maofisa ugani wengine wakiwamo wa ngazi za kata na wamejipangia ratiba ya kazi zao za kila siku ikiwamo kutembea kila nyumba kuwahudumia wakulima na wenye bustani ndogo na kuwa karibu nao.

Ofisa Kilimo Mkuu kutoka ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Idara ya Tawala za Mikoa, Hoffu Mwakaje na Mkurugenzi msaidizi huduma za ugani katika Wizara ya Kilimo kwa nyakati tofauti wakabainisha matarajio yao ya matokeo chanya kwa wananchi baada ya uwezeshwaji huo.

Mwakaje alisema jitihada zote zinazofanywa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo, hazitakuwa na maana kama maofisa ugani hao watashindwa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Katibu Tawala Msaidizi, Uchumi na Uzalishaji, Mkoa wa Morogoro, Dk. Rosalia Rwegasira, alisema awali ukosefu wa vifaa ulisababisha taaluma yao kutoheshimika, tofauti na ofisa ambaye akiitwa huvaa mavazi ya kazi na vifaa, ofisa kilimo yeye huenda kawaida na kutothaminika katika kazi yake kwa wananchi na kwamba vifaa wanavyopewa ikiwamo vipima udongo, vitaboresha shughuli za ugani.

# Maadili, utu, umoja vyasisitizwa malezi ya watoto

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Rehema Sombi, amewashauri wazazi na walezi kuwalea watoto kwenye msingi bora kimaadili, utu na kujali umoja wa kitaifa.

Kiongozi huyo alitoa wito huo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kitabu cha 'The First Female President' kilichoandikwa na mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mwanga Mpya Academy, Rafat Simba, chenye dhima ya kuhamasisha watoto kusimamia ndoto zao.

Rehema alibainisha kwamba jamii imegubikwa na tabia za watu wachache waliokosa uzalendo na kutumia fursa walizonazo kwenye jamii kuwa chanzo cha migogoro, kuchochea na kuvunja uaminifu wa taifa lao na kuvunja heshima za viongozi wa nchi.

"Kinachoshangaza hao viongozi wa jamii wanashindwa kutumia nafasi zao kukemea matendo yanayokwenda kinyume na maadili na uzalendo wa taifa letu, wanatumia matamshi yanayotweza utu kwa kiongozi wetu, badala yake wanasukuma ajenda za kushawishi mambo ambayo siyo mazuri," alisema na kuongeza;

"Watu hawa ambao wapo ndani ya jamii zetu wanashangaza sana, lakini yote hayo yanatokana na kutokuwa na msingi mzuri wa uzalendo, utu, umoja na namna ambavyo tunaweza tukawaandaa watoto kuja kuwa viongozi wazuri katika siku za usoni," alisema Rehema.

Pia aliwaomba wazazi na walezi kutokuwa miongoni mwa watu wa aina hiyo, kwa kulea watoto ambao mwisho wa siku watakuja kuvunja misingi inayojenga taifa, badala yake wawakuze katika namna ambayo watajali maadili ya kitanzania.

Alisema kuwa serikali inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu na sekta nyingine ili kuchagiza maendeleo ya sekta ya elimu na taifa kwa ujumla na kuhakikisha kwamba vizazi vinaendelea kuwa bora kwa awamu zingine zijazo.

"Niendelee kuwashauri wazazi na walezi kuwa wasimamizi bora kwa watoto wao, ili waweze kutambua vipaji walivyonavyo, kwa kuwa kubaini vipaji vyao itasaidia vijana kujiajiri na kupunguza tatizo la ajira, pia itachagiza kukuza uchumi wa taifa letu," alisema Rehema.

Hata hivyo, alisema faida nyingine ya kutambua mapema vipaji vya watoto, itasaidia kuwaepusha na kujiingiza katika makundi mabovu katika jamii, akitolea mfano panyarodi analolitaja kama kundi linaloenda kinyume na maadili ya kijana wa kitanzania.

Vile vile, alimpongeza Rafat kwa uthubutu wa kuandika kitabu kinachohamasisha watoto kufanya mambo yenye faida kwao na taifa, huku akimwahidi kwamba atakipeleka kitabu hicho katika mikutano mikubwa inayoongoza na Rais Samia Suluhu Hassan.

Naye Rafat alisema wakati akisoma darasa la kwanza alikuwa akijihusisha na shughuli mbalimbali zilizomsaidia kujenga uwezo wake wa kusoma na kuandika ikiwamo mashindano ya kusoma na kuandika taarifa kwa ufupi, ambayo yalimuwezesha kwa kiasi kikubwa kuandika kutabu hicho kwa ufanisi.

"Nilijitahidi kushiriki kwenye mashindano hayo kila wakati na hata niliposhindwa sikukata tamaa bali nilisonga mbele, hapo kuna kitu cha kujifunza ambacho ni kuhakikisha kutokukata tamaa hata kama unapitia magumu kiasi gani, kuwa mvumilivu songa mbele utafanikiwa," alisema Rafat.

## Vikosi Niger vyatakiwa kukaa kwa tahadhari

**NIAMEY,** NIGER

VIONGOZI wa mapinduzi ya Niger wameamuru vikosi vyake vya kijeshi kuwa katika tahadhari ya hali ya juu, wakitaja ongezeko la tishio la mashambulizi.

Jeshi hilo lilisema agizo hilo lilikuwa kuruhusu vikosi vyake kujibu ipasavyo iwapo kutatokea shambulio lolote.

Jenerali Abdourahamane Tchiani, kiongozi wa mapinduzi, alisema kuwa Niger haitaki vita, lakini itajilinda dhidi ya uingiliaji wowote wa kigeni.

Alitia saini makubaliano na wanajeshi wenzake nchini Mali na Burkina Faso kuingilia kati nchini Niger iwapo kutatokea shambulizi.

"Ikiwa shambulio litafanywa dhidi yetu, haitakuwa kama matembezi katika bustani baadhi ya watu wanaonekana kufikiria," alionya.

Jumuiya ya Kanda ya Afrika Magharibi (ECOWAS) imekuwa ikitumia njia za kidiplomasia kubadili mapinduzi lakini ilisema iko tayari kutumia nguvu kama suluhu la mwisho.

Juhudi hizo zimeungwa mkono na Marekani na Ufaransa, ambazo zote zina kambi za kijeshi nchini Niger.

Msaidizi wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani anayeshughulikia Masuala ya Afrika, Molly Phee, alikuwa Nigeria, ambako alikutana na maofisa wa ECOWAS, ikiwa ni ziara yake ya kwanza ya mataifa matatu na kuzitembelea Chad na Ghana.

Aidha, Waziri wa Mambo ya Nje aliyeteuliwa na Junta alimpa balozi wa Ufaransa Sylvain Itté saa 48 kuondoka nchini humo mwishoni mwa juma lililopita, akiishutumu Ufaransa kwa kutenda kinyume na maslahi ya Niger.

Kwa mujibu wa Al Jazeera, maelfu ya waandamanaji wanaounga mkono mapinduzi walikusanyika katika mji mkuu, Niamey, Jumamosi, wakipeperusha bendera za Niger, Algeria na Russia na kushutumu Ufaransa. **BBC**

## Wananchi Gabon wapigwa 'stop' kutoka nje

**LIBREVILLA,** GABON

MAMLAKA nchini Gabon imetangaza marufuku ya kutotoka nje usiku hadi asubuhi huku ikizima intaneti kwa lengo la kudhibiti upotoshaji kupitia mtandao, wakati wa upigaji kura ukimalizika nchini humo.

Waziri wa Mawasiliano, Rodrigue Bissawou alibainisha hayo jana, akieleza kwamba sababu ni kukabiliana na kusambaa kwa wito wa ghasia na taarifa za uongo. Hatua hiyo inafuata malalamiko ya upinzani kuhusu hitilafu zilizoshuhudiwa katika uchaguzi uliofanyika Jumamosi.

Msemaji wa muungano rasmi wa upinzani, Alternance 2023, alizitaja hatua hizo za serikali ya Gabon kama hatua zilizovuka mpaka na kwamba mamlaka hazitaki kuona maendeleo ya demokrasia nchi humo.

Mwishoni mwa juma lililopita raia walipiga kura nchini humo kumchagua rais, wabunge na madiwani, huku ikielezwa kuwa vituo kadhaa vya kupiga kura vilichelewa kufungiliwa.

Rais wa sasa Ali Bongo ambaye amekuwa madarakani kwa miaka 14 anatafuta kuchaguliwa kuhudumu kwa muhula wa tatu.
**BBC**

# Putin awaamuru Wagner kusaini kiapo kuitii Russia

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amewaamuru wapiganaji wa kundi la Wagner kutia saini kiapo cha kuitii serikali ya Russia baada ya ajali mbaya ya ndege iliyomuua kiongozi wa kundi hilo la mamluki, Yevgeny Prigozhin.

Putin alisaini amri hiyo inayoleta mabadiliko na ilianza kutekelezwa Ijumaa, baada ya Kremlin kusema kwamba madai ya nchi za Magharibi kuwa Prigozhin aliuawa kwa amri yake kuwa ni uongo.

Mamlaka ya usafiri wa ndege ya Russia, ilisema kwamba Prigozhin alikuwa ndani ya ndege binafsi iliyoanguka Jumatano jioni kaskazini magharibi mwa Moscow na hakuna abiria aliyenusurika katika ajali hiyo, ambayo ilitokea miezi miwili baada ya Prigozhin kuongoza uasi uliofeli dhidi ya wakuu wa jeshi.

Ilielezwa kuwa Rais Putin alituma salamu za rambirambi kwa familia za waliofariki katika ajali hiyo Alhamisi ya wiki iliyopita na kumzungumzia Prigozhin katika zama zilizopita.

Aidha, ilielezwa kuwa Putin kuweka kiapo cha lazima kwa wafanyakazi wa kundi la Wagner na makandarasi wengine wa jeshi binafsi ilikuwa hatua ya wazi ya kuweka makundi kama hayo chini ya udhibiti mkali wa serikali.
**VOA**




Wananchi wakipanga foleni kwa ajili ya kupiga kura katika uchaguzi wa rais mjini Libreville Gabon, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Marekani: Uchaguzi Zimbabwe haukukidhi viwango

**HARARE,** ZIMBABWE

UBALOZI wa Marekani mjini Harare umejiunga na waangalizi wengine wa uchaguzi kueleza wasiwasi wao kuhusu uchaguzi mkuu wa Zimbabwe, ukisema kwamba haukufikia viwango vya katiba ya nchi hiyo na miongozo ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Kwa mujibu wa kaimu msemaji wa Ubalozi huo, Rebecca Archer- Knepper uchaguzi mkuu wa Zimbabwe uliofanyika Agosti 15, haukukidhi viwango vya kimataifa na kwamba Washington ina matumaini kuwa Wazimbabwe watabakia kuwa na amani wakati tume ya uchaguzi inahesabu kura.

"Wakati siku za uchaguzi zilikuwa za amani, mchakato wa uchaguzi hadi hivi sasa haujakidhi viwango vya kikanda na kimataifa, tunashirikiana wasi wetu mkubwa sana kama ule ambao umeelezewa na SADC na ujumbe wa waangalizi wengine wa kimataifa.

"Taarifa ya SADC ya Agosti 25 ilielezea kuwa uchaguzi haukukidhi mahitaji ya Katiba ya Zimbabwe, Sheria ya Uchaguzi, Misingi na Miongozo ya SADC inayotawala kanuni za kidemokrasia katika uchaguzi," alisema Archer-Knepper.

"Tume hizo zimeelezea matatizo kwa uwazi, uhuru, haki na hadhi ya mchakato wa uchaguzi; masharti yasiyofaa juu ya haki ya uhuru wa kukutana na kushirikiana, uhuru wa kujieleza mambo ambayo yameelezewa kwenye katiba ya Zimbabwe na kuwaengua wagombea, hasa wanawake," alisema Archer-Knepper. Christopher Mutsvangwa, msemaji wa chama tawala wa (ZANU-PF) aliwajibu waangalizi wa SADC kuhusu ukosoaji wao kwa uchaguzi, akieleza kuwa katika misingi ya SADC, wanataka kuweka bayana, kuwa ni matokeo ya mataifa wanachama wa jumuiya hiyo.

"Hayatekelezwi na kila mwanachama binafsi ambaye anakuwa mkuu wa ujumbe. Si wajibu wa mtu fulani maalum kujitwika mwenyewe jukumu la kutathmini kamati ya katiba ya sheria za Zimbabwe. Kwa hiyo Nevers

Mumba kutoka Zambia, tunakueleza wewe. Usiingilie sheria za Zimbabwe," alisema Mutsvangwa.

Mkuu wa Tume ya Uangalizi ya SADC kwa uchaguzi wa Zimbabwe,

Nevers Mumba, alisema ada ya dola 20,000 ya kujiandikisha kuwa mgombea uraia ilikuwa ni kubwa mno, alielezea pia kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Zimbabwe kusita kutoa orodha ya wapigakura kwa upinzani kwa muda muafaka na kukosoa kuvurugwa kwa mikutano ya uchaguzi ya wapinzani kulikofanywa na polisi.

Waziri wa Sheria wa Zimbabwe, Ziyambi Ziyambi, alielezea uungaji mkono wake kwa taarifa za Mutsvangwa.
**VOA**

# NBC YASHIRIKI WOGGING YA AMREF, YATOA MILIONI 200/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imeungana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wadau wengine kushiriki mbio fupi zilizoambatana na matembezi ya hiari (Wogging), zilizoandaliwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Afya Zanzibar na Shirika la Kimataifa la Amref Afrika, Tawi la Tanzania zikilenga kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga visiwani humo.

Kupitia tukio hilo ambalo ni sehemu ya Kampeni ya 'Uzazi na Maisha', benki hiyo pia ilitoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 200 vitakavyotumika kwenye hospitali mbalimbali za Zanzibar ili kuboresha huduma ya afya.

Akizungumza baada ya kushiriki matembezi hayo yaliyoanzia eneo la Kiembe Samaki kwa Butros Wilaya ya Magharibi B na kumalizikia viwanja vya Maisara, Zanzibar, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wakubwa na Wateja wa Serikali Benki ya NBC, Linley Kapya, alisema mbali na mazoezi ya viungo, ushiriki wa benki hiyo ulilenga kuunga mkono jitihada za Serikali za kupunguza na kuepusha vifo vya kinamama wajawazito na watoto wachanga ambapo bado kiwango cha changamoto hiyo kipo juu.

"Kama ambavyo amebainisha Rais Dk. Mwinyi kwamba takwimu zinaonesha kuna vifo vya kina mama 134 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka na vifo 28 vya watoto wachanga kati ya vizazi hai 1,000 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017. Hali hiyo husababishwa na changamoto za huduma duni za mama na mtoto katika hospitali na vituo vya afya zikiwamo uhaba wa wahudumu na tatizo la kukosekana kwa dawa.

"NBC tukiwa wadau tunaosapoti sekta zote ikiwamo michezo na afya tukaona ni vema kwetu tukiwa sehemu ya jitihada hizi muhimu kushiriki," alisema.

Kwa mujibu wa Kapya mbali na michezo, benki hiyo imekuwa mdau mkubwa wa afya visiwani humo ambapo imekuwa ikitoa huduma za vipimo bure kwa wamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano kupitia programu yake ya Mobile Clinics kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ya Zanzibar.

Akizungumza kwenye tukio hilo pamoja na kuzungumzia umuhimu wa mazoezi kiafya sambamba na kuwapongeza washiriki wa wogging hiyo, Dk. Mwinyi, alieleza matumaini yake kupitia kampeni hiyo, ni kwamba serikali itaongeza vifaa tiba kwa vituo vya afya 28, sawa na asilimia 40.5 ya vituo vyote 69 vinavyotoa huduma za mama na mtoto Zanzibar.

Kwa upande wa Naibu Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Hafidh, alisema lengo la kuanzishwa kwa kampeni ya "Uzazi ni Maisha" inayohusisha michezo ni kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto nchini.

Naye Mkurugenzi mkazi wa Shirika la Amref Afrika Tanzania, Dk. Florence Temu, pamoja na kuwashukuru wadau mbalimbali walioshiriki kwenye kampeni hiyo, alisema lengo la kuanzishwa kampeni hiyo ya "Uzazi ni Maisha" ni kukusanya shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununuliwa vifaa tiba vya hospitali na vituo vya afya 69 vinavyotoa huduma za mama na mtoto Zanzibar.

"Tukiwa kwenye mwaka wa pili wa kampeni hii, Shirika la Amref tayari tumefanikiwa kukusanya Sh. milioni 557 na tumepokea ahadi za Sh. milioni 883 ambayo itafikisha lengo la kampeni hii kufikia 2024," alibainisha.




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa tatu kushoto), akikabidhi chetu cha shukrani na utambuzi kwa Mkuu wa kitengo cha wateja wakubwa na wateja wa serikali wa Benki ya NBC, Linley Kapya (wa pili kulia), kutambua mchango wa benki hiyo katika kufanikisha kampeni ya 'Uzazi na Maisha' iliyoambatana na mbio fupi zilizoambatana na matembezi ya hiari (Wogging), ambazo zilifanyika Zanzibar mwishoni mwa wiki. Benki hiyo ilitoa msaada wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 200 kufanikisha kampeni hiyo. Wengine ni pamoja na Naibu Waziri wa Afya, Zanzibar Hassan Hafidh (kushoto), Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Amref Afrika Tanzania, Dk. Florence Temu (kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# *Mashujaa kwenda Burundi kusaka mechi*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah 'Bares' amesema atatumia mapumziko ya wiki tatu ya Kalenda ya FIFA kuendelea kukinoa kikosi chake ikiwa ni pamoja na kupata mechi tatu za kirafiki nchini Burundi.

Akizungumza jana kutoka Kigoma, kocha huyo alisema hiki ni kipindi ambacho anataka kukiweka kikosi chake sawa kwani kina wachezaji wengi wapya na wengine ambao hawajawahi kucheza hata mechi hiyo.

"Wachezaji wetu tumewapa siku tatu tu za mapumziko baada ya hapo watarejea na kuanza programu za mazoezi kwa ajili ya mechi za kirafiki ambazo zitatupa ukomavu kwenye ligi, kama unavyoona timu yetu bado ngeni, ina wachezaji baadhi wapya na wengine hawajabahatika kucheza hata mechi moja ya ligi, tunahitaji kuwapa uzoefu ili wote wawe imara," alisema.

Alisema mechi tatu tu zinamtosha ili kuweka kikosi chake kwenye hali njema ya mapambano wakati Ligi Kuu itakaporejea.

"Kwangu mimi nahitaji mechi tatu, zinatosha sana, ila nataka zile zenye ushindani na tumeona ndugu zetu wa Burundi timu zao nazo zinajiandaa kwa ajili ya ligi, hivyo wameitikia wito wa kutaka kucheza na sisi mechi za kirafiki, kwa hiyo ningependa kucheza na timu za huko, kama itapatikana nafasi ya wao kuja sawa, lakini sisi wenyewe tunaweza kwenda huko kucheza," alisema.

Mpaka sasa Mashujaa iliyopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu huu, haijapoteza mechi yoyote, ikishinda mechi ya kwanza mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar na suluhu dhidi ya Geita Gold.

# Tunda Man ataka shule ziibue vipaji

**Na Mwandishi Wetu**

Mwanamuziki Khaleed Ramadhan maarufu Tunda Man, ameshauri shule ziwe na programu za kuibua vipaji vya vijana.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati akitumbuiza kwenye mahafali ya Shule ya Sekondari ya Brilliant ya Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam.

Alisema mbali na masomo, kuna umuhimu kwa shule kutenga muda wa michezo na burudani kwani kwa kufanya hivyo wataibua vipaji vingi na watu maarufu kwa siku za usoni.

Tunda Man aliibua shangwe kwa wanafunzi wa shule hiyo mara tu mshereheshaji wa tukio hilo alipotangaza uwapo wake kwenye mahafali hayo.

Aliposhuka kwenye gari lake wanafunzi walishindwa kujizuia na wote walivamia katikati ya uwanja na kuanza kuimba naye nyimbo mbalimbali ukiwamo ule wa naipenda 'Naipenda Simba Sihami Hata Mniue'.

Tunda mbali na kuimba wimbo maarufu wa 'Naipenda Simba Sihami Hata Mniue' aliimba nyimbo mbalimbali za kupongeza mafanikio ya timu ya Yanga hali iliyoibua furaha na shangwe kwa wanafunzi wa timu zote mbili.

Aidha, aliwataka wanafunzi wa shule hiyo wasome kwa bidii ili waweze kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya kidato cha nne inayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka huu.

# Coastal yashusha ndugu wa Modric

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache kabla ya dirisha la usajili kufungwa, klabu ya Coastal Union imemsajili mchezaji Fran Golubic raia wa Croatia.

Klabu hiyo pia imemteua Abbas el Sabri kuwa Ofisa Habari wake badala ya Jonathan Tito ambaye ameteuliwa kuwa Meneja wa Mashindano wa klabu hiyo.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo inasema imemsajili mchezaji huyo mwenye uwezo wa kucheza beki wa kulia, kushoto, kiungo mkabaji na winga zote mbili.

"Tumemsajili kwa miaka miwili nyota wa Croatia, Fran Golubic mwenye uwezo wa kucheza beki wa kushoto, kulia, kiungo mkabaji na winga zote," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DOUCOURE AWINDWA LIVER

KIUNGO wa kati wa Crystal Palace na Mali, Cheick Doucoure mwenye umri wa miaka 23, yuko juu ya orodha ya Liverpool inayosaka kiungo mpya na thamani yake ni pauni milioni 70. (***Football Insider)***

### CUCURELLA ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United imewasiliana na Chelsea kuhusu kumnunua kwa mkopo mchezaji wa Hispania, Marc Cucurella, 26. (***Fabrizio Romano***)

### SALAH KWENDA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 31, ameiambia klabu hiyo anataka kujiunga na Klabu ya Saudi Arabia ya Al-Ittihad. (***Rudy Galetti***).

### TIERNEY SAFI ARSENAL

MLINZI wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 26, ametua Hispania kukamilisha uhamisho wa kwenda kwa mkopo Real Sociedad. (***Fabrizio Romano***)

### GALLAGHER AIKATAA SPURS

KIUNGO wa kati wa England, Connor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, atakataa kuhamia Tottenham Hotspur ili kupigania nafasi yake Chelsea. (***Football Insider***)

### ALMADA ATAKIWA AJAX

KLABU ya Ajax ipo kwenye mazungumzo na Atlanta United kuhusu dili la kiungo wa Argentina, Thiago Almada mwenye umri wa miaka 22. (***90 min***)

### FRIMPONG ALENGWA CHELSEA

CHELSEA inalenga kumnunua mlinzi wa Bayer Leverkusen na Uholanzi, Jeremie Frimpong mwenye umri wa miaka 22. (***Fichajes***)

### BALEBA KUTUA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imekubali ada ya pauni milioni 23.2 kumsajili kiungo wa kati wa Lille na Cameroon, Carlos Baleba, 19. (Sport)

### FRESNEDA HUYOOO LISBON

MLINZI wa pembeni, Ivan Fresneda mwenye umri wa miaka 18, anatarajiwa kujiunga na Sporting Lisbon kutoka Real Valladolid. Alihusishwa na Arsenal na Newcastle United. (***Fabrizio Romano***)

### BARCA NA FRESNEDA

BARCELONA pia walikuwa wakimtaka Ivan Fresneda, lakini wakachagua kumsajili Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 29 kutoka Manchester City. (***Athletic***)

### EZE MKATABA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inaweza kumpa kiungo wa kati wa England, Eberechi Eze mwenye umri wa miaka 25, mkataba wa pauni milioni 5 kwa mwaka na kifungu cha kutolewa kwa mkopo huku kukiwa na nia kutoka Manchester City. (Sun)

### LENGLET AULIZIWA SEVILLA

SEVILLA wameuliza kuhusu uwezekano wa kumsajili tena mlinzi wa Ufaransa, Clement Lenglet mwenye umri wa miaka 28 kutoka Barcelona. (***Marca)***

### AMRABAT HAKIELEWEKI

KOCHA wa Fiorentina, Vincenzo Italiano, anaitaka bodi kutafuta suluhu na kiungo wa kati wa Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27 licha ya Manchester United kumtaka. (***Sky Germany***)

# DONDOO ZA SOKA

## MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG AKUNWA USHINDI NA KIWANGO MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amesifu timu yake kwa kumaliza mwanzo mbaya baada ya kuifunga Nottingham Forest mabao 3-2 katika mchezo wa kusisimua wa Ligi Kuu England pale Old Trafford kwenye Ligi ya England, Jumamosi.

**Wenyeji walikuwa nyuma kwa mabao 2-0 yakifungwa na Taiwo Awoniyi na Willy Boly na kuwafanya wageni hao kuwa mbele.**

Lakini Christian Eriksen akafunga na Casemiro kisha mkwaju wa penalti wa Bruno Fernandes ukawawezesha 'Mashetani Wekundu' hao kuondoka na pointi tatu.

"Ni jambo la kutisha kuanza kuwapa mabao mawili na kufanya makosa, lakini nimefurahishwa sana na kurejea mchezoni," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Uongozi, jinsi tulivyotulia na kufunga, nina imani na mabadiliko makubwa ndani ya kikosi cha Man United.

> Tumecheza mpira mzuri sana, nje ya mpango na kanuni na sheria tulifunga mabao mazuri...

"Tulicheza mpira mzuri sana, nje ya mpango na kanuni na sheria tulifunga mabao mazuri."

United walianza msimu wa Ligi ya England kwa kufungwa bao 1-0 na Wolverhampton Wanderers, na pia wakachezea kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Tottenham Hotspur wiki iliyopita.

Hivyo, ushindi wa Jumamosi ulikuwa faraja kubwa kwa kikosi hicho cha Ten Hag na kurudi kwenye njia kuu za Ligi Kuu England.

"Kila timu mwanzo ina maeneo ambayo inabidi iboreshe na sisi tunayo, tunatakiwa kusonga mbele pale unapotaka kupata mafanikio," alisema.

"Kuna ari kubwa katika timu hii, wamepata njia ya kushinda."

Nahodha Fernandes alikuwa mwenye hamasa na Ten Hag hakuacha kumsifu kiungo huyo wa Ureno.

"Katika nyanja zote alicheza mchezo mzuri sana katika kiwango cha juu, akiwa mtulivu, akitumia hisia zake kwa wakati sahihi, alikuwa na uwezo wa kushambulia, akifanya mabadiliko, alifurahishwa sana na uchezaji wake," alisema.

Kulikuwa na majeruhi mmoja kwenye ushindi huo baada ya beki Raphaël Varane kulazimika kutolewa nje baada ya kuumia.

"Alikuwa na malalamiko, hatukutaka kumhatarisha, tuna Harry Maguire, Victor Lindelöf, ambaye angeweza kuchukua nafasi yake, ili tusianguke hatarini."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 689

MECHI KALI

AZAM
VERSUS
TANZANIA PRISONS

1 | 1.53
X | 3.82
2 | 5.78

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## ARTETA AMTETEA HAVERTZ KWA MASHABIKI WA ARSENAL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amemtetea Kai Havertz baada ya mashabiki wa Arsenal kumshutumu kucheza chini ya kiwango katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Fulham Jumamosi.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 67.5, majira ya joto kutoka Chelsea, aligusa mpira mara chache zaidi (22) kuliko mchezaji yeyote wa Arsenal katika kipindi cha kwanza na alitolewa dakika 56 na timu yake ikiwa nyuma kwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Emirates.

Kikosi cha Arteta kilijibu bao la Andreas Pereira la dakika ya kwanza kwa mabao mawili ndani ya dakika tatu.

Bukayo Saka alisawazisha kwa mkwaju wa penalti na Eddie Nketiah aliyetokea akaiweka Arsenal mbele kabla ya Calvin Bassey wa Fulham kutolewa nje kwa kadi nyekundu zikiwa zimesalia dakika saba mpira kumalizika.

Lakini bao la João Palhinha dakika ya 88 liliwanufaisha wageni na Arteta alipuuza kile kilichoonekana kuwa ni kufadhaika kutoka kwa mashabiki wa nyumbani kilichoelekezwa kwa uzembe wa Havertz - haswa alipopoteza mpira muda mfupi kabla ya kutolewa.

"Niliona kitendo alipocheza nyuma na angeweza kugeuka," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Hiyo ni zaidi nadhani mahitaji ya kila mtu kucheza mbele na kuathiri mchezo katika tatu ya mwisho kwa sababu tulikuwa na umuhimu wa kushinda."

Havertz hana bao au asisti katika mechi tatu hadi sasa na mashabiki wameonekana kutomuunga mkono na Arteta alisema: "Ndiyo nadhani hivyo. Nadhani tayari amefanya mambo mazuri sana.

"Leo ilikuwa ngumu katika nyakati fulani. Aliingia katika maeneo makubwa na mpira haukufika. Katika hali nyingi alipaswa kufunga mabao mengi tayari msimu huu. Hicho ndicho kitu ambacho kinakosekana huko."

Arteta alisisitiza kuwa timu yake ilifanya vya kutosha kushinda mchezo huo licha ya kutocheza vizuri na kuruhusu mabao mawili duni.

"Jinsi timu ilivyocheza, jinsi timu inavyozalisha, mchezo mwingine wowote unashinda kwa tofauti ya pointi 100," aliongeza.

"Lakini huu ni mpira wa miguu, tunatoka sare na tumeruhusu mabao mawili duni sana leo (juzi). Hiyo ndiyo tofauti, kwenye Ligi Kuu unapotoa kitu kingine utapata adhabu. Tulikuwa leo.

"Wachezaji wa chini walifanya mabadiliko makubwa, athari kubwa, nilipenda dhamira na ujasiri walioleta kwenye timu. Tulifanya jambo gumu zaidi, kwenda mbele kwa mabao 2-1."

# Pulisic gari limewaka Milan

**MILAN,** Italia

CHRISTIAN Pulisic anaonekana kuwa na mwanzo mzuri zaidi kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, baada ya kufunga bao la pili kwenye mchezo wa pili mfululizo.

Baada ya kuifungia AC Milan bao la kwanza wikendi iliyopita, Pulisic pia alifunga katika mechi yake ya kwanza Uwanja wa San Siro na kuwafanya Rossoneri kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Torino kwenye Serie A Jumamosi.

Olivier Giroud alifunga penalti mbili na kufikisha mabao matatu katika mechi mbili za kwanza, huku Theo Hernández pia akifunga bao.

"Mechi bora, kazi ya kila wiki ilitufanya tuwe sawa," alisema Pulisic akiiambia DAZN.

"Timu imefanya mchezo kuwa mzuri na uimarishaji wa hali ya juu umefika. ... Kundi zuri linaundwa kwa mtazamo, upatikanaji."


Pulisic alihusishwa na mchezaji mwenzake wa zamani Giroud kufunga bao katika mechi yake ya kwanza huko Bologna na wakati huu alikuwa Ruben Loftus-Cheek aliyesaidia kutengeneza bao la kwanza dakika ya 33.

Pulisic alianza harakati hiyo katika eneo la kiungo kwa kumtengenezea mpira Loftus-Cheek.

Giroud hakuweza kuingia kwenye mkwaju, lakini ilimjia Pulisic, ambaye alikimbia na kufunga bao la kwanza.

Pulisic na Loftus-Cheek walijiunga kutoka Chelsea mwezi uliopita.

Perr Schuurs aliisawazishia Torino dakika tatu tu baadaye, lakini Giroud akarejesha bao kwa Milan kabla ya kipindi cha mapumziko kwa mkwaju wa penalti baada ya mlinzi wa Torino, Alessandro Buongiorno kucheza madhambi katika eneo la hatari.



,132,450

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/08/23 | 21:45 | Nottingham vs Burnley | 2.32 | 3.32 | 2.83 |
| 02. 31/08/23 | 02:30 | Charlotte FC vs Orlando City | 2.50 | 3.51 | 2.60 |
| 03. 31/08/23 | 03:30 | Racing Club vs Boca Juniors | 2.56 | 2.95 | 2.70 |
| 04. 31/08/23 | 19:00 | HJK Helsinki vs Farul Constanta | 2.19 | 3.20 | 3.20 |
| 05. 31/08/23 | 20:00 | Twente vs Fenerbahce | 2.17 | 3.45 | 3.05 |
| 06. 31/08/23 | 20:00 | Brann vs AZ Alkmaar | 3.11 | 3.36 | 2.17 |
| 07. 31/08/23 | 20:00 | Apoel Nicosia vs KAA Gent | 3.14 | 3.24 | 2.21 |
| 08. 31/08/23 | 21:00 | SC Dnipro 1 vs Spartak Trnava | 2.44 | 3.35 | 2.70 |
| 09. 31/08/23 | 21:00 | Adana Demirspor vs Racing Genk | 2.50 | 3.49 | 2.55 |
| 10. 31/08/23 | 21:00 | Partizani Tirana vs Astana | 2.47 | 3.23 | 2.74 |
| 11. 31/08/23 | 21:30 | FC Lugano vs Union Saint Gilloise | 2.60 | 3.30 | 2.55 |
| 12. 31/08/23 | 21:45 | Aberdeen vs BK Hacken | 2.65 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 31/08/23 | 22:00 | Zrinjski Mostar vs LASK Linz | 2.60 | 3.21 | 2.60 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 28/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4084 | PSM Makassar vs Persis Solo | 1.56 | 3.89 | 4.75 |
| 16:00 | 4747 | Muang Thong Utd vs Port FC | 2.19 | 3.43 | 2.77 |
| 16:30 | 5998 | Llantwit Major vs Llanelli AFC | 2.98 | 3.54 | 2.03 |
| 17:00 | 1340 | Tonbridge Angels vs Welling | 1.74 | 3.62 | 4.03 |
| 17:00 | 1644 | Halifax vs Gateshead | 2.46 | 3.35 | 2.63 |
| 17:00 | 2099 | Guiseley vs Bradford PA | 2.53 | 3.21 | 2.54 |
| 17:00 | 2280 | Eastleigh vs Aldershot | 2.04 | 3.41 | 3.30 |
| 17:00 | 2700 | York City vs Rochdale | 2.73 | 3.30 | 2.40 |
| 17:00 | 2770 | Truro City vs Farnborough Town | 2.14 | 3.40 | 2.95 |
| 17:00 | 3328 | Torquay vs Braintree | 1.57 | 3.93 | 4.79 |
| 17:00 | 4144 | Bognor Regis vs Lewes | 2.80 | 3.61 | 2.15 |
| 17:00 | 4733 | Woking vs Dorking Wanderers | 1.61 | 4.02 | 4.64 |
| 17:00 | 5421 | Bromley vs Southend | 2.83 | 3.25 | 2.36 |
| 17:00 | 5428 | St.Albans vs Bath City | 2.02 | 3.41 | 3.21 |
| 17:00 | 5830 | Oxford City vs Boreham Wood | 2.99 | 3.30 | 2.23 |
| 17:00 | 5928 | Barnet vs Ebbsfleet | 1.80 | 3.56 | 4.03 |
| 17:30 | 2475 | SK Super Nova vs FK Liepaja | 7.33 | 5.09 | 1.30 |
| 18:00 | 2764 | Pyunik Yerevan vs West Armenia | 1.07 | 8.56 | 20.39 |
| 18:30 | 1482 | Hermanstadt vs Universitatea Cluj | 2.21 | 3.09 | 3.19 |
| 18:30 | 3301 | KuPS Akatemia vs OLS Oulu | 3.10 | 3.66 | 1.98 |
| 19:00 | 4277 | Arsenal Tula vs Torpedo Moscow | 2.88 | 3.03 | 2.31 |
| 19:00 | 5783 | Azam vs Tanzania Prisons | 1.53 | 3.82 | 5.78 |
| 19:20 | 4176 | Al Orubah vs AL Ain | 2.16 | 2.95 | 3.15 |
| 19:30 | 2074 | Salernitana vs Udinese | 2.72 | 3.33 | 2.62 |
| 19:30 | 3195 | Hobro vs Sonderjyske | 3.49 | 3.69 | 1.81 |
| 20:00 | 1096 | CD Eldense vs Eibar | 2.88 | 2.93 | 2.49 |
| 20:00 | 1403 | Moss vs Kristiansund | 2.62 | 3.37 | 2.32 |
| 20:00 | 1456 | Nacional Madeira vs Leixoes | 2.14 | 3.23 | 3.13 |
| 20:00 | 2017 | Gais vs Skovde Aik | 1.36 | 5.01 | 7.51 |
| 20:00 | 3271 | Aris Limassol vs Doxa Katokopia | 1.48 | 4.11 | 6.24 |
| 20:00 | 3911 | Elfsborg vs Norrkoping | 1.49 | 4.05 | 5.26 |
| 20:00 | 4196 | AIK Football vs Varbergs Bois | 1.40 | 4.14 | 6.46 |
| 20:00 | 5470 | Vejle BK vs Brondby | 3.72 | 3.62 | 1.89 |
| 20:10 | 3010 | Sirius FK vs Malmo | 4.14 | 3.84 | 1.65 |
| 20:30 | 2825 | Getafe vs Alaves | 2.27 | 2.92 | 3.74 |
| 20:40 | 5994 | AL Bukayriyah FC vs AL Khlood | 2.70 | 2.80 | 2.55 |
| 21:00 | 1721 | Al Hilal Riyadh vs Al-Ettifaq | 1.22 | 6.06 | 11.49 |
| 21:00 | 3293 | Jong PSV vs Helmond Sport | 2.20 | 3.52 | 2.81 |
| 21:00 | 3405 | Al Raed Club vs AL Riyadh | 2.15 | 3.56 | 3.09 |
| 21:00 | 3805 | HK Kopavogs vs Vestmannaeyjar | 2.08 | 3.56 | 2.95 |
| 21:00 | 5101 | Giresunspor vs Bandirmaspor | 3.63 | 3.48 | 1.83 |
| 21:30 | 4941 | UTA Arad vs Steaua Bucuresti | 4.53 | 3.66 | 1.68 |
| 21:45 | 2304 | Treaty United vs Waterford Utd | 7.66 | 5.04 | 1.28 |
| 21:45 | 3012 | Cagliari vs Inter | 6.36 | 4.24 | 1.52 |
| 21:45 | 4365 | Annecy FC vs St Etienne | 3.34 | 3.39 | 2.02 |
| 22:00 | 3061 | FC Sarajevo vs Velez Mostar | 1.83 | 3.32 | 3.98 |
| 22:15 | 4836 | Rio Ave vs Porto | 6.76 | 4.37 | 1.41 |
| 22:30 | 1731 | Rayo Vallecano vs Atletico Madrid | 3.95 | 3.43 | 1.98 |
| 22:30 | 4822 | Racing Santander vs Huesca | 2.03 | 3.07 | 3.67 |
| 23:30 | 4005 | Barranquilla FC vs Bogota FC | 2.07 | 3.05 | 3.46 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MBUNGE MOSHI MJINI ATOA NENO MBIO ST MARY GORETI

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI za kielimu zikiwamo shule hususan zile za sekondari zimeshauriwa kutenga siku maalum kwa ajili ya michezo ikiwamo mbio ndefu za marathon ili kuwajengea vijana utamaduni wa kufanya mazoezi kujikinga na maradhi yasiyo ambukiza wakiwa na umri mdogo.

Ushauri huo umetolewa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro, Priscus Tarimo wakati wa mashindano ya St Mary Goreti School Marathon pamoja na matembezi ya hisani, yaliyofanyika katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na kuvutia zaidi ya washiriki 800 wakiwamo wanafunzi, walimu na wazazi.

"Michezo ikiwamo mbio ndefu ni muhimu katika kujenga afya, hivyo ni bora vijana wakaanza kujengewa tabia ya kushiriki michezo mbalimbali ili kuepuka magonjwa yasioambukiza kama vile maradhi ya moyo badala ya mtu kuanza mazoezi wakati ashakabiliwa na changamoto za kiafya," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa uongozi wa shule zingine na hata taasisi za elimu ya juu mkoani humo kuchukulia mashindano hayo yaliyoandaliwa na uongozi wa St. Mary Goreti School kama kielelezo cha kuanzisha mashindano katika maeneo yao.

"Uamuzi wa kuanzisha mashindano ya aina hiyo kwenye taasisi za elimu ziende sambamba na kuanzishwa kwa bonanza maalum la michezo kila mwaka ambalo litashirikisha wanafunzi kutoka shule mbalimbali kwa pamoja," alisema.

Aliongeza: "Bonanza la namna hiyo mbali na kujenga afya ya mwili pia litatumika kuendeleza umoja na ushirikiano miongoni mwa Watanzania wakiwa katika ngazi za shule kutokana na ukweli kwamba kutawaunganisha wanafunzi wanaotoka sehemu mbalimbali za nchi".

Kwa upande wa Mwenyekiti wa riadha mkoani Kilimanjaro (KAAA), Abraham Mikumi, aliupongezi uongozi wa St Mary Goreti School kwa kuandaa mbio hizo na matembezi ya hisani ambapo alitoa rai kwa wahusika kuangalia utaratibu wa kufanya tukio hilo kila mwaka.

"Sisi kwa utaalamu wetu tumeona mbio za leo ni fursa ambayo sisi kama viongozi wa riadhaa mkoani Kilimanjaro tunaweza kuitumia kuibua na kukuza vipaji vipya kwenye nyanja za riadha kutokana na matokeo ya walioshinda kwenye tukio la leo," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Shule hiyo, Sr Clementina Kachweka, Naibu Mkuu wa shule hiyo, Sr Cleopa Sarita, alisema mbio hizo na matembezi ya hisani yameandaliwa na uongozi wa shule hiyo kwa lengo la kuchangisha fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo.

"Tamasha hili ni sehemu ya matukio ambayo tunaendelea nayo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa shule hii, ambayo yanatarajiwa kufanyika mwakani," alisema.

Aliyataja matukio mengine mbali na uzinduzi uliofanywa hivi karubuni kuwa ni pamoja zoezi la upandaji miti maeneo mbalimbali mkoani humo, uchangiaji damu kwa wahitaji sambamba na uchunguzi wa afya kupitia kambi maalum iliyoandaliwa kwa ajili ya zoezi hilo.



Baadhi ya washiriki wa mbio za hisani na matembezi za Shule ya Sekondari ya St Mary Goreti wakianza mbio hizo katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) mwishoni mwa wiki. Mbio hizo ni sehemu ya maadhimisho ya jubilee ya miaka 25, tangu kuanzishwa kwa shule hiyo. **MPIGAPICHA WETU**.

# Gamondi aianzia kazi Al-Merrikh

INATOKA UK 24

katika mechi yetu ya leo (juzi).

"Tumecheza vizuri, lakini kama benchi la ufundi kuna mapungufu nimeyaona na naenda kuyafanyia kazi kukisuka kikosi na kuwa imara zaidi ya sasa," alisema Gamondi.

Kuhusu mechi iliyopita dhidi ya Asas FC, Gamondi alisema amefurahishwa na jinsi wachezaji wake walivyocheza kwa kufanyia kazi kile alichoelekeza kwenye uwanja wa mazoezi.

Alisema walicheza kwa umakini mkubwa kuanzia safu ya ulinzi, kiungo hadi ushambuliaji, lakini hakufurahishwa na kitengo cha Zawadi Mauya kucheza rafu ambayo ilisababisha penalti.

"Ni kweli sikupenda kitendo kile alichokifanya Mauya, nilimweleza mara kwa mara hata tunapokuwa kwenye mazoezi huwa namweleza makosa kama haya yanaigharimu timu, na sasa amesababisha kuruhusu kufungwa bao kwa penalti," alisema kocha huyo.

Aliongeza: "Natengeneza timu kwa kila mchezaji awe na uwezo wa kufunga, pia kucheza mpira mzuri ambapo utawasaidia mbeleni katika mashindano au mechi zilizopo mbele yao," alisema Gamondi.

Naye kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Maxi Mpia Nzengeli, alisema amefurahi kuona viongozi wa Yanga kumpa thamani kwa siku ya juzi kuipa kuita 'Max Day'.

Alisema hiyo ni ishara kubwa ya upendo kwa uongozi na mashabiki na kuhakikisha kuwa ataheshimu upendo huo na kupambania timu hiyo ifikie malengo yao ikiwamo kucheza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo kwa miaka mingi Yanga haijawahi kufika hatua hiyo.

Kocha wa Asas FC, Muwlid Ali Beilleh, alisema walishindwa kutimiza mipango yao baada ya kufanya makosa na Yanga kuyatumia na kuruhusu idadi kubwa ya mabao.

Alisema mechi hii waliingia kwa kufunguka kufanya mashambulizi tofauti na mechi ya kwanza ambayo waliruhusu mabao 2-0 baada ya kucheza kwa kuzuia zaidi.

"Tumekubali matokeo, niwapongeze wachezaji wangu kupambana na timu kubwa ambayo imecheza mpira mzuri na kufanikiwa kupata ushindi, katika mpira kuna mambo matatu, kufungwa, kushinda na sare, tumekubali kupoteza na tunaenda kujipanga kwa msimu mwingine," alisema Ali Beilleh.

# Michezo

Jumatatu Agosti 28, 2023

Nipashe


UK. 21



Ten Hag akunwa ushindi na kiwango




Chama

# Guu la kulia ni hatari mabao Ligi Kuu Bara

●●● Chama, Onana na Baleke waubeba mguu wa kushoto huku ya kichwa yakiwa...

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA mechi 13 za Ligi Kuu Bara zimeshapigwa hadi sasa, jumla ya mabao 29 yamezamishwa nyavuni huku yaliyofungwa kwa mguu wa kulia yakiwa mengi zaidi kuliko yaliyotokana na mguu wa kushoto na kichwa.

**Mabao hayo 23 yamefungwa ndani ya boksi na sita yamefungwa nje ya eneo la hatari huku mawili yakiwa ni kwa faulo na moja la kona.**

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu Michezoni cha Nipashe, mabao 18 yamefungwa kwa mguu wa kulia na saba yakifungwa kwa mguu wa kushoto wakati matatu yakiwa ya vichwa na moja la kujifunga mwenyewe kwa kipa wa Coastal Union, Justin Ndikumana kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Dodoma Jiji FC ambayo walilala 2-1.

Mabao ya faulo kwenye Ligi Kuu mpaka sasa yamefungwa na Ibrahim Ajibu kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar, zikitoka sare ya bao 1-1, Agosti 20, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, lingine likifungwa na Martin Kigi wa JKT Tanzania katika mechi iliyochezwa Agosti 15 dhidi ya Namungo, Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi na likiwa bao pekee, maafande wakishinda 1-0.

Maguri wa Geita Gold ndiye mchezaji pekee kwenye Ligi Kuu aliyefunga bao lililotokana na mpira wa kona.

Ilikuwa katika mechi ya ufunguzi wa ligi hiyo msimu huu dhidi ya Ihefu alipopachika bao pekee, akiunganisha kwa kichwa mpira wa kona uliyopigwa na Edmund John.

Mabao sita katika mechi hizo 13 yaliyofungwa nje ya kisanduku cha hatari, Ajibu akiwa mchezaji pekee aliyefunga bao kwa umbali mrefu zaidi akifanya hivyo kiasi cha takriban mita 35 katika mechi ambayo timu yake ya Coastal Union ilicheza dhidi ya Mtibwa Sugar, huku mengine yakizamishwa na Kigi wa JKT Tanzania, Meshack Abraham wa Dodoma Jiji, Adam Adam na Othman Dunia wote wa Mashujaa na Mudathir Yahaya wa Yanga.

Wakati wachezaji 16 wakiongozwa na Feisal Salum wa Azam FC na Mathew Antony wa Mtibwa Sugar kila mmoja wakifunga mawili, wakipachika 18 kwa mguu wa kulia kwenye ligi mpaka sasa, jumla ya wachezaji saba wamefunga mabao saba kwa kutumia mguu wa kushoto.

Wachezaji hao ni Clatous Chama, Willy Onana na Jean Baleke wote wa Simba, Adam Adam na Othman Dunia wa Mashujaa FC, Hija Ugando wa Coastal Union na Rashid Chambo wa KMC.

## Gamondi aianzia kazi Al-Merrikh

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutinga raundi ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Angel Gamondi amesema sasa ni muda wa kufanya maandalizi ya mchezo uliopo mbele yao dhidi ya Al-Merrikh ya Sudan.

Yanga juzi ilifanikiwa kusonga mbele baada ya kushinda mabao 5-1 dhidi ya As Al Sabieh (Asas FC) kutoka Djibouti, katika mchezo wa marudiano uliopigwa Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, hivyo kusonga mbele kwa ushindi wa jumla wa mabao 7-1, kutokana na mchezo wa awali kushinda 2-0.

Mabao ya Yanga juzi yalifungwa na Max Nzengeli dakika saba na 90, Hafiz Konkoni (dk. 45), Pacome Zouzoua (dk. 55) na Clement Mzize (dk. 69), huku bao la Asas FC likifungwa na Tito Mayor kwa mkwaju wa penalti dakika ya 85.

Kwa matokeo hayo Yanga sasa itakutana na Al-Merrikh ya Sudan, katika mchezo wa kwanza utakaopigwa hapa nchini kati Septemba 15-17, mwaka huu kabla ya marudiano nchini Rwanda, ambapo miamba hiyo ya Sudan inacheza mechi zake za nyumbani kutokana na kwao kukumbwa na machafuko ya kisiasa.

Akizungumza baada ya dakika 90 za mchezo huo kukamilika, Gamondi alisema wanatumia siku moja kusherehekea ushindi dhidi ya Asas FC na baada ya hapo watakuwa na kazi kubwa ya kujiandaa na mechi yao ijayo dhidi ya Al-Merrikh.

Alisema anaifahamua Al-Merrikh ni timu kubwa na wanauzoefu wa mashindano hayo, hivyo wanatakiwa kufanya maandalizi mazuri ya kutafuta ushindi mechi ya nyumbani na baadaye kumaliza kazi ugenini.

"Tumemaliza hatua hii tumesonga mbele, lakini tuna kazi kubwa mbele yetu kushinda mechi zote mbili na kutinga hatua ya robo fainali, tunaenda kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042